# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

### MFUMO WA UPANGAJI MIPANGO SHIRIKISHI JAMII WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO

## KITABU CHA REJEA




S.L.P 1923
DODOMA

Novemba, 2007

# YALIYOMO

**ORODHA YA VIFUPISHO ........ III**

**UTANGULIZI ........ IV**

**1.0 USULI ........ 1**

1.1 HISTORIA YA UPANGAJI MIPANGO KATIKA TANZANIA ........ 1

1.2 JUHUDI ZA USHIRIKISHWAJI WANANCHI KATIKA KUPANGA ........ 3

**2.0 DHANA ZA MIPANGO ........ 4**

2.1 MIPANGO NA BAJETI ........ 4

2.2 MIPANGO YA UWIANO ........ 5

2.3 UPANGAJI MIPANGO SHIRIKISHI ........ 7

2.4 MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO ........ 8

2.5 MAPITIO NA UWEZESHAJI ........ 9

**3.0 MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO ........ 13**

3. 1 SIFA ZA MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO ........ 13

3.2 MIONGOZO YA SERA NA MIKAKATI YA KITAIFA ........ 15

*3.2.1 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ........ 15*

*3.2.2 Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini ........ 17*

*3.2.3 Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) 18*

3.3 MASUALA MTAMBUKA ........ 21

*3.3.1 Jinsia na Maendeleo ........ 21*

*3.3.2 Utawala Bora ........ 25*

*3.3.3 Haki za Binadamu ........ 26*

*3.3.4 UKIMWI ........ 31*

*3.3.5 Menejimenti ya Mazingira ........ 36*

*3.3.6 Maafa ........ 38*

3.4 MAANDALIZI YA KIJAMII ........ 41

3.5 MAPITIO NA UWEZESHAJI ........ 45

3.6 DHANA ZINAZOTUMIKA KATIKA MCHAKATO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO ........ 45

**4.0 MCHAKATO WA KUANDAA MIPANGO SHIRIKISHI JAMII KWA MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO ........ 47**

4.1 Itifaki ya Kuingia katika Jamii na Maandalizi ya Kijamii ........ 47
4.2 Uzinduzi wa mchakato wa upangaji mpango shirikishi Jamii ........ 51
4.3 Ukusanyaji wa Takwimu ........ 52
*4.3.1 Takwimu za Mazingira ........ 53*
*4.3.2 Takwimu za Nyakati ........ 55*
*4.3.3 Takwimu za Kijamii na Kiuchumi ........ 57*
4.4 Kuandaa Rasimu ya Mpango Shirikishi Jamii ........ 69
4.5 Kikao maalum cha Halmashauri ya Kijiji ........ 71
*4.5.1 Kuweka vipaumbele kwa malengo mahususi ........ 71*
*4.5.2 Halmashauri ya Kijiji kuandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu ........ 73*
4.6 Kamati ya Maendeleo ya Kata ........ 74
4.7 Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji ........ 75
4.8 Muhtasari wa shughuli za utekelezaji kisekta ngazi ya Kata ........ 75
4.9 Ufuatiliaji na Tathmini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 76

**KIAMBATISHO 1: MCHAKATO WA MJINI ........ 77**

**KIAMBATISHO II: RATIBA YA MCHAKATO WA KIJIJINI ........ 80**

**KIAMBATISHO III: RATIBA YA MCHAKATO WA MJINI ........ 82**

**KIAMBATISHO IV: FOMU YA TAKWIMU ........ 84**

**Orodha ya Vifupisho**

| | | |
|---|---|---|
| JICA | : | Japan International Cooperation Agency |
| KMK | : | Kamati ya Maendeleo ya Kata |
| LEPSA | : | Learner-centred, Problem-posing and Self Analysis |
| LGA | : | Local Government Authority |
| MKUKUTA | : | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| MTEF | : | Medium Term Expenditure Framework |
| NAPC | : | National Aids Control Program |
| O&OD | : | Opportunities and Obstacles to Development |
| OWM-TAMISEMI | : | Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa |
| PRA | : | Participatory Rural Apraisal |
| RAS | : | Regional Administrative Secretary |
| RCC | : | Regional Consultative Committee |
| RDC | : | Regional Development Committee |
| RPFB | : | Rolling Plan Forward Budget |
| SARAR | : | Self-esteem, Associative Strengths, Resourcefulness, Action-planning, and Responsibility |
| UKIMWI | : | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | : | United Nations Development Program |

## UTANGULIZI

Ushirikishaji Wananchi katika kupanga na kutekeleza mipango yao wenyewe ni falsafa inayohimizwa na kutekelezwa katika nchi nyingi duniani hasa zile za ulimwengu wa tatu. Hapa nchini, Sera na miongozo mbalimbali vinatoa kipaumbele juu ya ushirikishwaji wananchi katika maendeleo yao. Baadhi ya Sera na miongozo hii ni pamoja na: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Sera ya Maendeleo Vijijini, pamoja na Mwongozo wa Taifa wa Bajeti.

Ushirikishwaji Wananchi unazofaida nyingi ambazo ni pamoja na Wananchi kumiliki maendeleo yao; Miradi inayotekelezwa kuwa endelevu; Kuongezeka kwa uwajibikaji wa Wananchi na Viongozi wa Serikali;Kuongezeka kwa uwazi katika kutoa maamuzi; Kupungua kwa gharama za Serikali za kutoa huduma kwa Wananchi kutokana na michango yao katika utekelezaji wa miradi; na kwa mujibu wa Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ushirikishwaji wa Wananchi unalenga kutoa madaraka zaidi kwa Umma katika maamuzi.

Kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa kunakotokana na Sheria Na. 7 – 10 za mwaka 1982 kunalenga kutekeleza azma ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa umma na kuboresha utoaji wa huduma bora. Maboresho ya Sekta ya Umma na yale ya Serikali za Mitaa ambayo yanaendelea kutekelezwa, yanalenga kuongeza ufanisi na uwezo wa Sekta ya Umma katika utoaji wa huduma bora kwa lengo la kuondoa umaskini katika jamii.

Kwa muda wote, upangaji mipango nchini umemilikiwa na kuongozwa na Wataalam wa Serikali, Wahisani na Washirika wa maendeleo ambao daima wamekuwa na hisia za udhibiti na kwamba wao wanajua mahitaji ya Wananchi na Wananchi hawayajui mahitaji yao. Mwenendo huu umepelekea mipango mingi iliyoanzishwa, kuwa na malengo ambayo hayaendani na matakwa ya jamii na hivyo kudumaza uhuru wa jamii kutoa maamuzi, na kutokuwa endelevu.

Kutokana na mapungufu haya, Serikali imebuni Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo mwaka 2001.Mfumo huu unazo sifa zifuatazo:

- Mfumo wa upangaji mipango unaanzia chini kwenda juu
- Unaanza kwa utambuzi wa fursa ili kukabiliana na Vikwazo vya maendeleo ndani ya jamii kwa kutumia fursa zilizopo na hivyo kujenga tabia ya kujitegemea.
- Unafanya kazi katika muundo wa Serikali za Mitaa na kuendana na mfumo wa upangaji mipango na bajeti wa kitaifa
- Unawawezesha jamii kuandaa mipango yao kwa kutumia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025
- Mfumo unazingatia uwiano wa kisekta katika ugawaji wa rasilimali.

Maboresho katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yameharakisha kuenezwa kwa Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa maendeleo kwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania bara tangu ulipoanzishwa mwaka 2001. Mwezi Machi Mwaka 2004, Serikali ilitoa mwongozo kwa ajili ya kuanzisha na kueneza Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama msingi wa kugatua madaraka kwa Wananchi, kuimarisha demokrasia, kuhimiza haki za binadamu na kuondoa umaskini.

Pamoja na mwongozo kuonyesha mahitaji ya Mapitio na Uwezeshaji wa mipango ya Jamii, utaratibu unaowezesha mchakato wa upangaji mipango kuwa endelevu haujaanzishwa. Katika mazingira haya, mwaka 2006 mwezi Juni Serikali iliendesha uchunguzi wa mfumo ili kuuboresha mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa maendeleo na kuweka utaratibu wa Mapitio na Uwezeshaji. Shirika la Maendeleo la Japan- JICA liliiwezesha Serikali kufanya zoezi hilo. Kutokana na matokeo na mapendekezo ya uchunguzi, Serikali imefanya marekebisho kadhaa katika mchakato wa kueneza mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na pia imeamua kuweka utaratibu wa Mapitio na Uwezeshaji.

Vitabu vya awali vya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo yaani , Rejea, Kiongozi cha Mkufunzi, Kiongozi cha Mwezeshaji Kijijini na Mjini vimerekebishwa ili kulingana na mabadiliko. Pia kitabu kipya kimetayarishwa ili kuwezesha uelewa wa matumizi ya utaratibu wa Mapitio na Uwezeshaji kama kiambatisho cha kitabu cha Rejea.

Mwisho, ninapenda kuchukua fursa hii kushukuru kwa michango iliyotolewa na Wadau mbalimbali wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na Wizara mbalimbali za Kisekta na kulifanya zoezi hili kuwa la mafanikio.

Tarishi, M.K.
**Katibu Mkuu**
Novemba, 2007

# 1.0 USULI

## 1.1 Historia ya Upangaji Mipango katika Tanzania

Tangu tupate Uhuru mwaka 1961, Serikali ilidhamiria kuwa na mchakato shirikishi wa wa upangaji mipango ya kiuchumi, ili kuwa na mfumo wa upangaji unaotoka chini kwenda juu. Juhudi za Serikali za kutekeleza dhamira hii zinaweza kuangaliwa katika hatua mbalimbali zilizochukuliwa kushirikisha Jamii katika kujiletea maendeleo yao. Juhudi hizi zinaweza kuangaliwa katika awamu kuu tatu;-

- Kipindi cha 1961 – 66 (Mara baada ya Uhuru
- Kipindi cha 1967 – 92 (Azimio la Arusha)
- Kipindi cha 1992 – 2002 (Kipindi cha Maboresho)

**Kipindi cha kwanza** 1961 – 66, Kiliongozwa na Dira ya Uhuru iliyolenga kuboresha maisha ya wananchi kwa kupigana na maadui watatu; **ujinga, maradhi na umasikini**. Jamii ilihimizwa kufanya kazi kwa bidii na kufanya shughuli za maendeleo kwa kujitolea kama mchango wao katika ujenzi wa Taifa. Kauli mbiu ya UHURU NA KAZI ilitumika kwa kuhimiza watu. Kauli mbiu hii ilisisitizwa zaidi na Hayati Mwalimu Julius K.Nyerere aliyehitimisha kwa kusema "Inawezekana; timiza wajibu wako". Ni katika kipindi hiki ambapo utawala wa kiimla wa Machifu ulivunjwa ili kuwezesha wananchi kuwa na madaraka katika utoaji wa maamuzi.

**Kipindi cha pili,** 1967 – 1992 Kiliongozwa na Azimio la Arusha. Falsafa ya kujenga uchumi wa Jamii kwa msingi wa "Ujamaa na kujitegemea" ilikuwa ndio lengo la Kitaifa la maendeleo la muda mrefu. Mkakati wa utekelezaji wa Azimio la Arusha, pia ulilenga kupeleka madaraka kwa wananchi. Matokeo yake, Serikali za Mitaa za utawala wa Kikoloni zilivunjwa mwaka 1972, ili kutoa nafasi ya kuanzishwa kwa madaraka Mikoani. Chini ya utaratibu huu, Serikali za Vijiji, Kamati za Maendeleo za Wilaya na Kamati za Maendeleo za Mikoa zilianzishwa; ili kuwezesha ushirikishaji zaidi wa Jamii katika utoaji wa maamuzi. Hatua hii ilitokana na sheria ya Madaraka Mikoani ya mwaka 1972.

Ili kuimarisha mfumo wa kupeleka madaraka kwa Jamii, Serikali za Mitaa zilianzishwa upya kwa sheria na. 7 – 10 ya mwaka 1982. Hii ni kutokana na katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara za 145 na 146 zinaruhusu mamlaka ya Serikali za Mitaa kupeleka madaraka kwa Jamii. Serikali za Mitaa zina haki na mamlaka ya kushiriki, na kushirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika maeneo yao.

**Kipindi cha tatu,** 1992 – 2002 kilitawaliwa na maboresho ya sekta ya Umma. Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (Bara) ilifanya maboresho kwa ajili ya kuongeza ufanisi na uwezo wa sekta ya umma katika utoaji huduma bora. Maboresho yamejikita katika maeneo yafuatayo;-

- Maboresho ya Utumishi katika Serikali kuu
- Maboresho ya Serikali za Mitaa
- Maboresho katika sekta ya fedha
- Maboresho katika sekta ya sheria
- Maboresho katika upangaji mipango na baajeti
- Maboresho katika mashirika ya Umma
- Maboresho ya muundo wa Tawala za Mikoa

Shabaha za maboresho haya ni kuleta mabadiliko ya majukumu ya Serikali kuu kutoka yale ya Serikali hujihusisha moja kwa moja na utekelezaji, uzalishaji mali na utoaji huduma na kuwa yale ya kuandaa sera, kuratibu, kushauri, na kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, watu binafsi na mashirika yasiyo a kiserikali. Aidha, kujenga mazingira yanayowezesha Serikali na wananchi kushirikiana kuboresha utendaji wa kazi kwa upande mmoja na Serikali za Mitaa kuwa na majukumu ya utekelezaji na usimamizi wa shughuli zote za maendeleo, utoaji huduma, utawala wa kisheria na uimarishaji demokrasia ili kurahisisha maendeleo ya wananchi.

Ingawa Serikali iliendelea kuweka mazingira mazuri ya ushirikishwaji kama ilivyoelezwa hapo juu bado ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutoa maamuzi uliendelea kumilikiwa na Maafisa Mipango/Wachumi, warasimu na wafadhili ambao wana hisia potofu za udhibiti na ufanisi wenye msingi wa "tunajua (wataalamu) hawajui (Jamii)" kwa hiyo, Ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutoa maamuzi haukutekelezwa kikamilifu. Huko nyuma wananchi walihusishwa tu kwa kutumia njia zifuatazo;-

**i. Chakula kwa kazi**

Chakula kwa kazi ni utaratibu wa kuhusisha wananchi katika shughuli mbalimbali za maeneo ama kwa kujitolea na kupewa chakula au kwa mtindo wa mkopo kwa mkopo (Kopa ngombe lipa ngombe). Kwa utaratibu huu baadhi ya matatizo yanaweza kutatuliwa; na miradi inaweza kukamilika kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

**ii. Uchangiaji Gharama.**

Utaratibu huu una lengo la kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuwahusisha walengwa. Azma ya utaratibu huu ni kuondokana na utoaji wa huduma za bure, na kujenga utamaduni wa kuhakikisha kuwa huduma hizi zinamilikiwa na wananchi wenyewe na zinakuwa endelevu. Mfano huu wa uchangiaji gharama hutumika katika huduma za Jamii kama vile maji, elimu, afya n.k.

***iii. Mkataba na Walengwa***

Utaratibu huu unaonyesha mahusiano kati ya walengwa na wahisani/Serikali ambapo Jamii inatakiwa kuchangia kukamilisha mradi ambao mhisani/Serikali imefanya sehemu iliyoahidi. Mara nyingi kunakuwapo na makubaliano kati ya walengwa na wahisani juu ya kukamilika kwa mradi. Utaratibu huu hutumika sana katika miradi ya ujenzi wa barabara, shule, vituo vya afya na maji.

## 1.2 Juhudi za Ushirikishwaji Wananchi katika Kupanga

Kumekuwepo na majaribio mbalimbali ya kutumia mbinu shirikishi katika baadhi ya maeneo hapa nchini, hususan katika miradi iliyofadhiliwa na wahisani. Baadhi ya mbinu shirikishi zilizotumika katika jitihada hizi ni pamoja na: PRA, SARAR, ZOOP na LEPSA[1]. Kwa kiwango fulani, mbinu hizi shirikishi zimewezesha Jamii kufanya maamuzi katika mchakato wa upangaji. Hata hivyo mbinu hizi zote zilikuwa zikiegemea zaidi katika kubaini matatizo hivyo basi kuongeza mategemeo ya Jamii kwamba watapewa misaada mara moja kutoka nje kutatua matatizo yao. Hali hii inajenga tabia tegemezi, pia mara nyingi miradi ya wafadhili inayotumia mbinu shirikishi inakuwa tayari inayo malengo yao tofauti na yale yanayoibuliwa na wananchi; hivyo kutoa nafasi ndogo sana kwa Jamii kujiamulia yale wanayotaka.

Kwa mapungufu hayo, Juhudi hizi ziliishia kwenye kuwahusisha tu wananchi badala ya kuwashirikisha, kwa ujumla upangaji katika Tanzania umeendelea kubaki kuwa ule wa kutoka juu kwenda chini tofauti na mategemmeo ya Serikali.

Matarajio ya Serikali kuimarisha upangaji yalikuwa kama ifuatavyo:

- Kuongeza ushiriki wa wananchi
- Kuwa na mipango ya uwiano
- Kuwa na upangaji wa kutoka chini kwenda juu

Mfumo wa upangajji Shirikishi wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo unatoa njia ambayo itasaidia Serikali kufikia matarajio haya.

---

[1] PRA ni ufupisho wa Participatory Rural Appraisal; SARAR ni ufupisho wa Self esteem, Associative strengths, Resourcefulness Action-planning and Responsibility; LEPSA ni ufupisho wa Learner Centered, Problem-posing and Self Analysis; ZOOP ni ufupisho Objective Oriented Planning (hii ilitumiwa na GTZ mwanzo mwa miaka ya 1980)

# 2.0 DHANA ZA MIPANGO

## 2.1 Mipango na Bajeti

Upangaji mipango ni mchakato unaoweka malengo, kubainisha rasilimali zilizopo/uwezo na mikakati itakayotumika kufikia malengo katika kipindi maalumu. Mara uandaaji wa mpango unapokamilika kinachofuata ni utekelezaji. Katika utekelezaji baadhi ya malengo yaliyowekwa katika mpango yanafikiwa na mengine hayafikiwi katika muda uliokusudiwa. Pia kadiri wakati unavyoenda ndiyo vipaumbele vipya vinavyoibuka kutokana na mabadiliko katika nyanja za kijamii na kiuchumi na sera. Hivyo basi, ipo haja ya kufanya mapitio mara kwa mara ili kuihuisha mipango, kwa kubaini utekelezaji ulipofikia na kuingiza vipaumbele vipya. Kwa msingi huu, mapitio ni sehemu muhimu katika mchakato wa upangaji mipango.

***Madhumuni ya kupanga***

- Kuwezesha utekelezaji wa shughuli katika utaratibu unaokubalika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.
- Kuweza kufahamu rasilimali zilizopo ili kukabiliana na Vikwazo.
- Kuweza kubinisha mahitaji ya Jamii.

***Faida za kupanga***

- Kupanga kunawezesha mgawanyo muafaka wa rasilimali chache zilizopo
- Kupanga kunawezesha utekelezaji wa shughuli kwa wakati.
- Mpango ni zana inayoongoza katika usimamizi wa shughuli za maendeleo.

**Njia za Uaandaji mipango**

Zipo njia kuu mbili za upangaji mipango, ambazo ni; Mipango inayotoka juu kwenda chini na ile ya kutoka chini kwenda juu.

Njia ya kutoka juu kwenda chini imezoeleka sana Tanzania. Njia hii ina sifa zifuatazo:

- Huweka shabaha, malengo na mikakati
- Huweka mwongozo wa kupanga katika ngazi mbalimbali
- Huweka ukomo wa matumizi ya fedha
- Huweka muda maalum wa utekelezaji

Kwa ujumla njia ya kupanga mipango kuanzia juu kwenda chini ina sifa isiyofaa ya kuihusisha Jamii badala ya kuwawezesha watu ili waweze kushiriki katika utoaji wa maamuzi yanayohusu shughuli zao za maendeleo. Aidha njia hii ina tabia ya kuwafanya watu kuwa tegemezi kwa Serikali.

Njia ya pili ya kupanga mipango ni kwa kuanzia chini kwenda juu, nayo inaonekana katika sura mbili:

- Sura ya kwanza ni pale ambapo Jamii inatumia zana shirikishi kuibua vipaumbele vilivyotokana na msukumo wa nje ya Jamii. Mipango yenye sura hii pia inaleta utegemezi.
- Sura ya pili ni ile ambayo Jamii inaongoza na kufanya maamuzi katika mchakato wa kupanga. Sura hii inajenga hisia za umiliki.

**<u>Bajeti</u>**

Bajeti ni sehemu ya mchakato wa upangaji mipango. Bajeti inahusisha mgawanyo wa rasilimali chache katika shughuli za maendeleo zilizopangwa. Bajeti inawezesha utekelezaji shughuli zilizopangwa kwa hiyo, mipango na bajeti inategemeana, mpango bila bajeti hauwezi kutekelezeka hata kama, ni mzuri kiasi gani.

***Mahusiano kati ya mipango na Bajeti***

| **Mpango** | **Bajeti** |
|---|---|
| Ni zana ya usimamizi | Zana ya usimamizi |
| Huweka malengo | Kuchambua vyanzo vya mapato |
| Hutambua rasilimali na matumizi yake | Huweka mgawanyo wa matumizi ya mapato |
| Hutoa ufafanuzi | |

### 2.2 Mipango ya Uwiano

Mipango ya uwiano inasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa ushirikiano kati ya wadau mbalimbali katika kushughulikia mahitaji ya Jamii. Mipango ya uwiano inadhibitisha kwamba mahitaji ya Jamii yana upana mkubwa hivyo utekelezaji toka kwa watu mbalimbali ni muhimu ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mathalani kuzuia vifo vya akina mama wajawazito ni lengo la afya, katika Kijiji Fulani pamoja na mambo mengine linahitaji:

- Kuboresha kilimo (mazao na mifugo) ili kuhakikisha ulaji wa chakula bora na cha kutosha (sekta ya kilimo)
- Kuboresha barabara ili kuwezesha wajawazito kufika kwenye huduma za afya bila matatizo (miundombinu)
- Utoaji wa hudumu bora kwa wajawazito kupitia vituo vya afya wataalamu wa huduma za uzazi na ukunga (Sekta ya Afya)
- Kuwaelimisha wanaume juu ya haja ya kuwajibika zaidi na kutokuwaachia kina mama kufanya kazi nzito na hasa mama anapokuwa mjamzito (utamaduni)
- Kutoa elimu kwa wanaume na wanawake kuhusu uzazi wa mpango (Elimu, Afya)
- Upatikanaji wa huduma za maji ili kuwapunguzia wanawake umbali wa kutembea wakitafuta maji (Sekta ya maji)

Kwa hiyo mipango ya uwiano ni mchakato ambao utekelezaji wa sera na mikakati ya sekta mbalimbali unalenga kufikia lengo la moja lililokusudiwa.

Faida za kuwa na mpango wa uwiano ni kama zifuatazo:

- Kuepuka kuichanganya Jamii
- Inapunguza kurudiarudia shughuli
- Inawezesha kubadilishana uzoefu
- Inakuza mahusiano kisekta
- Inaokoa muda
- Inawezesha matumizi mazuri ya rasilimali chache zilizopo.

**Mahusiano ya kisekta**

Mahusiano ya kisekta ni msingi wa kuwa na mipango ya uwiano. Hata hivyo, sekta mbalimbali mara nyingi zinashindwa kuwa na mahusiano kwa sababu zifuatazo;-

- Ubinafsi na kiburi cha wataalamu
- Watendaji kutokuwa na ufahamu na uelewa
- Uongozi mbaya
- Ukosefu wa mipango ya pamoja katika ngazi zote
- Migongano ya kimaslahi.
- Kubadilika badilika kwa sera
- Rasilimali zisizotosha.

### 2.3 Upangaji Mipango Shirikishi

Upangaji mipango shirikishi huiwezesha Jamii kutoa maamuzi katika mchakato wa uchambuzi, upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini ya mipango. Wakati wa mchakato Jamii huwezeshwa kujadiliana na kushauriana juu ya masuala yao ya maendeleo.

Upangaji mipango shirikishi unalenga;-

- **Watu**: Jamii hukusanya takwimu kwa kutumia zana shirikishi, kuchambua, kupanga na kuweka vipaumbele.
- **Vitendo:** Jamii humiliki mchakato wa kupanga, kutekeleza na matokeo.
- **Uwiano kisekta:** Shughuli za kiuchumi hutegemeana hivyo katika mchakato wa upangaji, masuala ya maendeleo yaangaliwe kwa pamoja (kwa ujumla wake).




Upangaji mipango shirikishi Jamii lazima uzingatie mambo yafuatayo:

- Jamii lazima ishirikishwe katika mchakato wa upangaji.
- Makundi yaishiyo katika mazingira magumu lazima yashirikishwe katika kutoa maamuzi. Makundi hayo ni pamoja na wazee, yatima, wajane, na walemavu.
- Kuhakikisha kuwa mchakato unafahamika na kueleweka vizuri na katika Jamii, Kata, Halmashauri za Serikali za Mitaa na wadau wengine wa maendeleo.

## 2.4 Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo

Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni mchakato wa upangaji shirikishi ambao unatumiwa hapa Tanzania kwa kuondoa mapungufu mengi ya mbinu nyingine za upangaji mipango shirikishi. Mfumo huu unazo sifa muhimu zifuatavyo:

- Una mtazamo chanya kwa Jamii: Katika mchakato Jamii huibua/ainisha fursa zilizopo ndani au nje ya maeneo yao ili kukabiliana na vikwazo vilivyopo katika kujiletea maendeleo, hali hii hujenga na kuinua ari ya kujitegemea.
- Mfumo huu unatumia zana shirikishi Jamii ambazo ni: Ramani ya Kijiji; Kata ya njia; Kalenda ya msimu, Uchambuzi wa Taasisi, Kalenda ya Kutwa Kijinsia, na Tathimini ya Uwezo wa Kujikimu wa Kaya, Makundi Mahsusi na Uchambuzi wa Vyanzo vya Mapato na Matumizi. Zana shirikishi nyingine zinazotumika ni Ramani ya Umilikaji Rasilimali Kijinsia na Uchambuzi wa Shughuli za Kiuchumi na Kijamii na athari zake Katika Mazingira.
- Unatumia bao mantiki ambalo huwezesha Jamii kuainisha kwa mantiki malengo mahsusi fursa, vikwazo, sababisho, ufumbuzi na hatua za utekelezaji. Pia Jamii inafanya uchambuzi rahisi wa vyanzo vya mapato na matumizi yake, hivyo kuweza kuamua yale wawezayo kufanya na yale wasioyaweza. Jamii pia huweka vipaumbele kulingana na mahitaji na uwezo wake na kutayarisha mpango wa miaka mitatu.
- Mfumo huu unamtazamo mkubwa wa kujitegemea na unasaidia Jamii kuzitambua rasilimali walizo nazo na jinsi ya kuzitumia vizuri. Kwa hakika unasisitiza umuhimu mkubwa wa kujitegemea.
- Mchakato unatumia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kama mwongozo wa jumla wa kisera.
- Kinachopatikana baada ya mchakato ni mpango wa jumla na siyo mpango wa kazi.
- Mfumo huu una mchakato wa Kijijini na Mjini.

Serikali inaamini kuwa mfumo huu utaongeza ari ya kujitegemea; kukusanya rasilimali vitu na rasilimali watu na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ;-

- Kupanga
- Kufanya maamuzi.
- Utekelezaji na usimamizi wa shughuli za maendeleo.

Mfumo huu umeingizwa katika muundo wa utendaji wa Serikali za Mitaa. Umeandaliwa kukidhi wajibu wa Serikali wa kupeleka madaraka kwa wananchi kama ilivyotamkwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekelezwa katika maboresho yanayoendelea ya Serikali za Mitaa. Kwa kufanya hivi Serikali inalenga kurejesha ari ya kujitegemea, kuhamasisha na kukusanya rasilimali za ndani, uwazi na uwajibikaji kwa kuhakikisha ufanisi katika ushirikishwaji wa Jamii katika kupanga kufanya maamuzi, kutekeleza na hivyo kumiliki shughuli za maendeleo yao.

Sifa nyingine za mfumo huu ni:

- Ni rahisi kumilikiwa na Jamii kuendesha mchakato wa kupanga mpango shirikishi kwa sababu unatumia zana shirikishi chache na rahisi kueleweka.
- Ni mfumo unaoleta uwazi na uwajibikaji
- Ni mfumo unaoziwajibisha Serikali kuu na Serikali za Mitaa kushauri na kusimamia mambo yaliyoamuliwa na wananchi wenyewe.
- Ni mfumo unaozisaidia Serikali za Mitaa kuratibu shughuli za wadau wengine wa maendeleo.
- Unajenga uwezo wa Jamii kushughulikia masuala mtambuka.
- Mfumo unaimarisha mahusiano kati ya Halmashauri za Wilaya na Sekretariet za Mikoa.

### 2.5 Mapitio na Uwezeshaji

Kupanga hakuishii kuwa na mpango tu. Kwa kawaida mchakato huendelea katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini na pia kuhuisha mpango, ambavyo vimo kwenye hatua ya mapitio ya mpango. Kwa upande wa upangaji katika Jamii, Halmashauri ya Wilaya ndiyo inayowezesha uwezeshaji na uimarishaji wa shughuli za maendeleo katika Jamii. Dhana ya *Ufuatiliaji na Tathmini* inaelezewa hapa chini

**Ufuatiliaji**

Ufuatiliaji ni utaratibu wa mara kwa mara wa kuangalia jinsi rasilimali zinavyotumika na hatua za utekelezaji ili kupata matokeo, mathalani unapojenga nyumba, unafuatilia kazi ya ujenzi na matumizi ya vifaa vya ujenzi. Ufuatiliaji unawezesha watekelezaji kuwa na taarifa zitakazotumika katika mkakati wa utoaji maamuzi katika mchakato wa kutekeleza mradi. Vipengele vya ufuatiliaji ni pamoja na matumizi ya fedha na maendeleo ya utekelezaji wa mradi kimaumbile, maendeleo ya fedha na utawala na ushiriki wa wadau(watekelezaji na wawezeshaji)

**Tathimini**

Tathimini ni upimaji unaofanyika kwa vipindi maalum ili kupima kazi iliyofanyika, matokeo na manufaa au mapungufu. Tathimini pia huweza kutoa taarifa zitakazojulisha kama:

- Manufaa ya mradi yamewafikia walengwa
- Shughuli za mpango zimekidhi matarajio na matakwa ya walengwa
- Malengo ya mradi yaliyowekwa yalikuwa halisi
- Kuna matokeo ambayo hayakutarajiwa yanayotokana na utekelezaji wa shughuli za mradi.

Katika ufuatiliaji na tathimini ni muhimu kuweka viashiria rahisi vinavyoeleweka vizuri. Viashiria vinapima utekelezaji ikilinganishwa na malengo. Taarifa ya maendeleo lazima ioneshe mchakato na matokeo ya viashiria.

Jedwali lifuatalo linaonesha Uhusiano kati ya ufuatiliaji na tathimini

**Ufuatiliaji na Tathimini**

| Ufuatiliaji | Tathimini |
|---|---|
| - Huhakikisha matumizi mazuri ya vifaa vya mradi<br>- Huhakikisha utendaji wa shughuli/kazi za kila siku<br>- Huangalia/kuona ratiba ya shughuli. | - Huangalia/kuona matokeo ya utekelezaji wa shughuli za mradi<br>- Hufanya upimaji wa utekelezaji kwa vipindi maalum<br>- Hupima matokeo halisi ikilinganishwa na malengo |

Zana za Ufuatiliaji na Tathimini:

- Mpango wa kazi
- Taarifa za maendeleo kama vile taarifa za kila mwezi, robo na mwaka ambao zina taarifa za maendeleo na matokeo ya mpango wa utekelezji
- Mkutano wa mapitio
- Kufanya ziara katika maeneo husika

**Kielelezo: Ngazi za Ufuatiliaji na Tathmini Shirikishi (Kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Mkoa)**



***Ufuatiliaji na Tathimini Shirikishi***

Ufuatiliaji na tathimini shirikishi ni mchakato ambao Jamii inashiriki kwa uchangamfu katika zoezi la ufuatiliaji na tathimini. Ni upimaji wa utekelezaji wa mpango wa Jamii chini ya juhudi za Jamii yenyewe. Ushirikishwaji unaleta uwiano katika mchakato wa ufuatiliaji na tathimini hivyo unatoa njia mpya za upimaji na kujifunza kutokana na mabadiliko zaidi yanayojumuishwa na yenye uwajibikaji kuelekea mahitaji na matarajio ya Jamii. ufuatiliaji na tathimini shirikishi umejikita siyo tu katika kupima ufanisi wa utekelezaji wa mipango, bali pia katika kujenga umiliki na kuiwezesha Jamii, kujenga uwajibikaji na uwazi vilevile, kuchukua hatua sahihi za kurekebisha ili kuboresha utendaji na matokeo. Upimaji na tathimini shirikishi umegawanyika katika sehemu mbili, ufuatiliaji shirikishi, na tathimini shirikishi.

**Kwanza,** Ufuatiliaji shirikishi ni mchakato wa utaratibu wa kuangalia rasilimali zilivyotumika na hatua za utekelezaji zilizofikiwa katika mpango. Mabadiliko yatokanayo na matumizi ya/rasilimali ili kuleta matokeo yanapimwa kwa kuzingatia vipengele muhimu vifuatavyo;

- Rasilimali Fedha,
- Utawala,
- Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa shughuli zilizobainishwa kwenye mpango,
- Nguvukazi iliyotumika katika utekelezaji

Hivyo basi ufuatiliaji shirikishi unalenga kuchambua manufaa au mapungufu na maendeleo, matokeo yake ni kupata mawazo ya kuboresha utekelezaji wa mpango.

**Pili,** Tathimini shirikishi ni upimaji wa mafanikio ya mpango unaofanyika katika ngazi ya Jamii kwa vipindi maalum. Ni mchakato wenye utaratibu unaopima mafanikio ya matokeo yakilinganishwa na vigezo vilivyowekwa katika mpango na namna vinavyohusiana na mafanikio au madhara kwa Jamii kwa hiyo tathimini shirikishi ni ufunguo wa kuweza kudhihirisha ishara na matokeo ya utekelezaji wa mpango wa Jamii.

**Ishara na matokeo**

Ishara ni vitu vinavyoshikika au huduma wakati wa utekelezaji katika mfumo wa mpango. Ishara zinahusika na kukamilika kwa shughuli Fulani maalumu katika hatua za utekelezaji. Mfano wa matokeo ni kama vile mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima au kukamilika kwa chumba cha darasa.

Matokeo yanatafsiriwa kama mabadiliko halisi au yaliyokusudiwa katika malengo yaliyoainishwa kwenye mpango. Matokeo yanaeleza kiwango cha mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa mpango, kwa kubainisha hatua zilizofikiwa katika malengo mahsusi.

Mfano; (Kama matokeo ya mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima mazao yameongezeka na/au kipato cha wakulima kimeongezeka. Kama chumba cha darasa kimekamilika, msongamano madarasani umepungua, mahudhurio ya wanafunzi yameongezeka hivyo utovu umepungua

## 3.0 MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO

### 3. 1 Sifa za Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo

Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni mchakato wa upangaji ulio makini na unaotumia zana shirikishi ili kuandaa mipango shirikishi Jamii kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kama mwongozo wa jumla wa kisera na hivyo kuwa msingi wa juhudi za kuondoa umaskini.

Mfumo huu wa upangaji umeingizwa katika muundo wa mamlaka wa Serikali za Mitaa. Mfumo huu umeandaliwa sanjari/na matarajio ya Serikali ya kutoa madaraka kwa Jamii kama ilivyo tamkwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekelezwa katika uboreshaji unaoendelea wa Serikali za Mitaa. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imerudisha moyo wa kujitegemea, ukusanyaji wa rasilimali za ndani, uwazi na uwajibikaji pale Jamii itakapo kuwa imeshiriki katika kupanga, kutoa maamuzi, utekelezaji na umiliki wa shughuli zao za maendeleo.

Ni mwanzo wa kuondokana na mfumo wa upangaji wa kutoka juu kwenda chini na kuwa wa kutoka chini kwenda juu. Kama ilivyoonyeshwa katika mchoro uliopo chini kushoto ni mfumo wa kutoka juu kwenda chini ambao hauna mfumo wa upangaji kati ya Halmashauri ya Wilaya na Jamii. Hali hii imeilazimu Serikali kuandaa mfumo Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ili kuziba pengo lililopo kama inavyoonyeshwa katika mchoro ulioko chini kulia.






Mchakato wa upangaji mipango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni wa ujumla na shirikishi. Mchakato wa upangaji unaanza kwa kuchagua makundi mbalimbali katika Jamii kwa kuzingatia jinsia umri na uwezo wa kiuchumi, ili kuhakikisha kuwa mawazo ya makundi yote katika Jamii yameingizwa katika mpango wa Jamii. Mojawapo ya shughuli muhimu sana inayofanyika wakati wa mchakato wa upangaji ni ukusanyaji wa Takwimu huu unasaidia watu kuelewa hali ya Jamii yao. Hivyo takwimu zilizokusanywa zitatumiwa na makundi mahsusi wakati wa kujadili malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kama mwongozo wa kuweka malengo mahsusi na kubainisha Fursa zitakazotumika kukabiliana na Vikwazo. Rasimu ya Mpango itapelekwa katika Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya kuweka gharama na vipaumbele. Halmashauri ya Kijiji itawasilisha Rasimu ya Mpango katika kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa ajili ya ushauri wa kitaalamu kabla ya kuwasilisha katika Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji kwa ajili ya kupitisha kama ilivyoelekezwa kisheria.

Mfumo huu una faida zifuatazo:

- Jamii inaweza kufuata mchakato wa upangaji kwa sababu unatumia zana shirikishi Jamii ambazo ni rahisi kufuata.
- Unaongeza uwajibikaji na uwazi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo siku hadi siku.
- Unaondoa utegemezi na kujenga tabia ya kujitegemea.
- Unachochea Jamii kumiliki matokeo yanayotokana na maamuzi yao.
- Unawajibisha Serikali kuu na Serikali za Mitaa kuwajibika kwa wananchi
- Unaweka msingi wa kuongoza Jamii katika kupunguza umaskini
- Unawezesha Halmashauri za Wilaya kuratibu shughuli za wadau wengine wa maendeleo.

## 3.2 Miongozo ya Sera na Mikakati ya Kitaifa

Upangaji Mipango Shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni kiungo muhimu kati ya jitihada za Jamii na Malengo Makuu yaliyoainishwa katika Miongozo ya Sera za Kitaifa, hususan Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA). Inaeleweka kuwa MKUKUTA ni mkatkati wa muda wa kati unaolenga katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo ndiyo msingi wa uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Jamii kwa Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inainisha malengo ya muda mrefu ambayo ni: Maisha Bora na Mazuri, Uongozi Bora na Utawala wa Sheria na Uchumi Imara unaohimili Ushindani. MKUKUTA unatafsiri malengo hayo makuu katika malengo ya muda wa kati kwa ajili ya utekelezaji chini ya nguzo pana tatu ambazo ni: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato; Kuboresha hali ya Maisha na Ustawi wa Jamii; na Utawala na Uwajibikaji. Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo unaiwezesha Jamii kutafsiri malengo mapana yaliyoainishwa katika miongozo hiyo ya kitaifa, kwenda kwenye malengo rahisi na yanayoeleweka kwa ajili ya kuandaa mipango yao.

### 3.2.1 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Kuanzia katikati ya miaka ya 1980 Serikali ilinga'mua kwamba miongozo na sera mbalimbali za maendeleo zilizokuwepo zilikuwa zimepitwa na wakati kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na kitekinologia yanayotokea katika Dunia. Kwa kuzingatia hilo Serikali mwanzoni mwa mwaka 1986 ilianza kuchukua hatua za kufanya maboresho katika snyanja za kiuchumi na kijamii i ambayo yanaendelea kutekelezwa hadi sasa. Hata hivyo ni dhahiri kwa Serikali na watu wake kuwa haya maboresho ya kijamii, na kiuchumi hayajaeleweka kwa usahihi kama falsafa ya Kitaifa yenye mwelekeo wa maendeleo ya muda mrefu.

Ni kutokana na uelewa huo umuhimu wa kuwepo kwa Dira ya Taifa ulijitokeza kama falsafa ya maendeleo ya mrefu. Serikali iliona umuhimu wa kurejesha matarajio ya watu, uzalendo na uraia na hivyo kuimarisha umuhimu wa kuwa na Dira ya Taifa. Dira ya maendeleo ni falsafa inayolenga kufikiwa kwa misha bora zaidi kwa Jamii. Hivyo dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kukusanya rasilimali watu na rasilimali nyingine ili kufikia malengo ya pamoja. Malengo ya pamoja yanaamsha matarajio ya watu na kuleta ari na msisimko wa kufikia maendeleo. Mchakato unaongeza ari na nia ya kukubiliana na changamoto kwa mtu binafsi, Jamii na Taifa. Dira ni chombo cha kuleta matumaini na chenye nia ya kuleta motisha kwa watu kupenda kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya ufanisi na ustawi wa Jamii.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inanuia kufikia maisha bora na mazuri kwa watu wake, kuwa na uongozi bora na wa kisheria na kujenga uchumi imara na wenye kuhimili ushindani. Imekusudiwa kuwa malengo yafuatayo yatakuwa yamefikiwa ifikapo mwaka 2025:

**(1) <u>Maisha bora na mazuri</u>**

Maisha bora na mazuri kwa kila mtanzania yanatarajiwa kupatikana kutokana na mikakati inayohakikisha kufikiwa kwa malengo yafuatayo:

- Kujitosheleza kwa chakula na uhakika wa upatikanaji wake
- Elimu ya msingi kwa wote, kufuta ujinga na kufikia kiwango kinachoridhisha cha elimu ya kati na juu kulingana na mahitaji ya kuwa na watenda kazi wenya uwezo wa kushughulikia kikamilifu changamoto za kimaendeleo katika ngazi zote.
- Usawa wa kijinsia na kuwapa fursa wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.
- Upatikanaji wa huduma bora za afya ya msingi kwa watu wote.
- Upatikanaji wa huduma bora za uzazi kwa watu wote wenye umri unaostahili.
- Kupunguza vifo vya watoto wachanga na vifo vya uzazi kwa robo tatu ya viwango vya sasa.
- Upatikanaji wa maji salama kwa watu wote.

**(2) <u>Uongozi bora na utawala wa kisheria</u>**

Inakusudiwa kwamba Jamii ya watanzania itakuwa na sifa zifuatazo:

- Maadili mema na kuthamini utamaduni.
- Uadilifu na kuheshimu utawala wa kisheria
- Kutokuwepo rushwa na maovu mengine
- Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengne na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo.

**(3) <u>Uchumi imara wenye kuhimili ushindani</u>**

Uchumi unatarajiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Kuwa na vianzio mbali mbali vya uzalishaji na uchumi ambao una maendeleo ya viwanda yaliyo karibu sawa na nchi zenye mapato ya kati.
- Utengemano wa uchumi unaojidhihirisha kwa kuwepo kwa kasi ndogo ya upandaji wa bei na uwiano madhubuti wa uchumi kwa jumla.
- Ukuaji wa uchumi kwa asilimia 8 au zaidi kwa mwaka

- Kuwepo kwa miundo mbinu ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya malengo ya Dira katika sekta zote
- Mshiriki na mshindani shupavu katika masoko ya nchi jirani na ya dunia kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kupenda na kuendeleza maslahi ya Taifa na kuwa na uwezo wa kujirekebisha haraka ili kuweza kubadili mabadiliko yanayotokea katika masoko ya nchi jirani na ya dunia.
- Kurekebisha hali ya sasa ya uharibifu wa mazingira na rasilimali (kama vile misitu, samaki, vianzio vya maji, hali ya hewa, udongo, na bionuai)

Pia inatarajiwa kwamba, ukuaji wa haraka utafikiwa iwapo ufanisi katika kugeuza hali iliyopo sasa ya upotevu na uharibifu wa rasilimali za mazingira kama vile misitu, samaki vianzo vya maji (bahari, mito, maziwa) Hali ya hewa ardhi, bionuai, na mkusanyiko wa kemikali zenye sumu kwa binadamu utafikiwa.

### 3.2.2 Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini

Tangu tupate Uhuru Taifa limekuwa likipambana na maadui watatu wa maendeleo ambao ni **Ujinga, Maradhi, na Umaskini.** Serikali ikishirikiana na Jamii imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ili kuondoa ujinga, maradhi, na umaskini. Pamoja na kuwepo juhudi hizo, bado nusu ya watanzania kimsingi ni maskini. Moja ya tatu yao wanaishi katika umaskini uliokithiri na kipato chao kwa siku kiko chini ya dola moja ya kimarekani ambacho hakiwezi kutosheleza mahitaji ya msingi kwa siku.

Viashiria vya umaskini ni pamoja na;-

- Kutojua kusoma na kuandika
- Uhaba wa maji safi na salama
- Huduma duni ya afya
- Vifo vingi vya akina mama na watoto
- Utapiamlo wa watoto na watu wazima
- Kipato duni
- Makazi duni
- Ukosefu wa ajira
- Kutofahamu maswala muhimu ya Jamii
- Mmomonyoko wa maadili
- Ukosefu wa amani na utulivu

### 3.2.3 Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA)

Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania maarufu kama MKUKUTA ulipitishwa na Bunge mwezi Februari 2005 kwa ajili ya utekelezaji katika kipindi cha miaka 5. MKUKUTA umechukua nafasi ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini. MKUKUTA umeandaliwa kwa kuzingatia ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na unalenga kufikia malengo ya Maendeleo ya Millennia. MKUKUTA unaangalia zaidi ustawi na utawala na ni chombo cha kukusanya juhudi na rasilimali na kupata matokeo yake. Sifa muhimu katika kuanzisha MKUKUTA zilikuwa umilikaji wa kitaifa na kushauriana na wadau hii ilipelekea mkakati kufikia matakwa ya wadau pamoja na maboresho ya mipango ya kisekta.

MKUKUTA unasisitiza kuangalia matokeo na unakusudia katika kuleta ushirikianao zaidi miongoni mwa sekta zote na wadau. MKUKUTA umeingiza maswala mtamuka kama vile jinsia, mazingira, ukimwi, wenye ulemavu, watoto, vijana, wazee, ajira, na makazi. Mkakati huu unalenga kuingiza umilikaji na kujumuisha uandaaji wa sera, ukijikita katika kuangalia sheria mila na desturi zinazodumaza maendeleo na zinazoathiri makundi ya wanyonge. Mkakati huu unahitaji nyongeza ya rasilimali na bajeti ya Serikali itapangwa kukidhi mahitaji ya MKUKUTA na muungano wa moja kwa moja na mapitio ya matumizi ya Serikali. Changamoto hii inahitaji mkakati wa pamoja wa kusaidia Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Hii itaongeza upeo na fanisi wa misaada ili kufikia malengo ya MKUKUTA.

**<u>Kanuni za MKUKUTA na muundo wake</u>**

MKUKUTA Umejengwa katika kanuni zifuatazo;-

- Umiliki wa kitaifa
- Utayari wa kisiasa kuhimiza demokrasia na haki za binadamu
- Uimarishaji wa uchumi wa kitaifa na maboresho ya kimuundo
- Ushirikishwaji wa mikakati ya kisekta
- Ushiriki wa wananchi katika mjadala wa sera
- Uratibu wa misaada
- Fursa sawa kwa watu wote
- Maendeleo endelevu
- Mahusiano ya uchumi mkubwa na ule wa ngazi za chini
- Kuunganisha masuala mtambuka

Mkakati unaainisha nguzo tatu zenye matokeo ya jumla

I. Ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini wa kipato.
II. Maisha bora na ustawi wa Jamii.
III. Utawala na uwajibikaji.

Kila nguzo ina shabaha na malengo mahsusi.

Il kufikia kila lengo mahsusi hatua za ufumbuzi zimeainishwa. Upo uhusiano mkubwa kati ya maeneo na yote yana umuhimu sawa. Kukua kwa uchumi kuna pelekea kukua kwa mapato hivyo kupunguza umaskini wa kipato. Kipato kikubwa huwezesha kaya kuboresha uwezo wa maisha kwa kupata elimu bora, afya, lishe na makazi
Uwezo wa binadamu ukiwa mkubwa uchumi huongezeka. Uchumi wa watu ukiwa mzuri huwezesha Serikali kukusanya kodi kwa ajili ya kuendeleza na kutoa huduma. Utawala bora husaidia hali salama na bora ya maisha na kupunguza umaskini.

**Muhtasari wa matokeo makuu tarajiwa na malengo ya maeneo makuu ya mkakati**

*Nguzo ya 1: Ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa Umaskini wa kipato*

**Matokeo ya Jumla:** Ukuaji unaozingatia matokeo kwa watu wengi na usawa unafikiwa na kuendelezwa.

Malengo:

- Kuhakikisha usimamizi mzuri wa uchumi
- Kukuza ukuaji wenye msingi mzuri wa uchumi
- Kuongeza upatikanaji wa chakula
- Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawake Vijijini
- Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawwke Mijini
- Kutoa nishati ya kuaminika na rahisi kwa watumiaji

*Nguzo ya 2: Maisha bora na ustawi wa Jamii*

**Matokeo ya jumla**

- Maisha bora na ustawi wa Jamii,pamoja na kuzingatia watu maskini sana na vikundi vinavyoweza kuathiriwa.
- Kupungua kwa tofauti za matokeo (mfano katika elimu; kuishi, afya) kunakozingatia masuala ya jiografia, kipato, umri, jinsia na vikundi vingine.
- Kuweka mfumo wa huduma za Umma.

Malengo:

1) Kuhakikisha upatikanaji sawa wa elimu bora ya msingi na sekondari kwa wavulana na wasichana Elimu ya watu wazima kwa wote miongoni mwa wanaume na wanawake, na upanuaji wa elimu ya juu, ufundi na elimu ya ufundi sadifu.
2) Kuboresha maisha, afya na ustawi wa watoto wote na wanawake na hassa vikundi vilivyo hatarini kudhurika.
3) Kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama makazi bora na mazingira salama na endelevu. Hii itapunguza udhurikaji unaotokana na athari za mazingira.
4) Kuhakikisha mifumo inayofaa kuruhusu upatikanaji wa huduma za umma zilizo bora na halisi kwa watu wote.
5) Kuhakikisha ulinzi wa kutosha wa Jamii na utoaji wa mahitaji muhimu na huduma kwa walio hatarini kudhurika na wenye shida.
6) Kuondoa unyanyasaji wa kijinsia.

*<u>Nguzo ya 3: Utawala na Uwajibikaji</u>*

Matokeo ya Jumla:

- Utawala bora na utawala wa sheria.
- Uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma.
- Demokrasia na kuvumiliana kisiasa na kijamii
- Amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano wa Jamii.

**Malengo**

- Kuhakikisha kuwa miundo na mifumo ya utawala pamoja na utawala wa sheria ni ya kidemokrasia, shirikishi, uwakilishi, uwajibikaji na unajumuisha watu wote.
- Kuhakikisha ugawaji sawa wa rasilimali za umma pamoja na kushughulikia tatizo la rushwa ipasavyo.
- Kuweka mfumo wa huduma za umma unaofaa
- Kuhakikisha kwamba haki za maskini na vikundi vilivyo hatarini kudhurika zinalindwa na kukuzwa katika mfumo wa haki.
- Kupunguza kutengwa na kutovumiliana kisiasa na Jamii.
- Kuboresha usalama binafsi na wa mali, kupunguza uhalifu na kuondoa unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji wa majumbani.

## 3.3 Masuala Mtambuka

### 3.3.1 Jinsia na Maendeleo

Kwa miaka mingi Serikali kwa hatua za makusudi ilidhamiria kujenga uwezo wa wanawake. Hii inatokana na ukweli kwamba wanawake wanamchango mkubwa katika maendeleo na utafutaji wa kipato na bado wanasahaulika. Utawala bora unasisitiza kuwepo kwa fursa sawa kwa wanawake na wanaume na pia maendeleo yanahitaji kutambua mahitaji maalum ya jinsia katika Jamii yatambulike.

***Kuelewa hali ya maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia jinsia***

Uingizaji wa jinsia katika mpango ni lazima uanzie hatua ya uchambuzi wa jinsia. Wakati wa mchakato wa upangaji Mipango Shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo, masuala ya jinsia ni lazima kuzingatiwa katika hatua ya kukusanya takwimu na uchambuzi wa hali. Wakati wa uchambuzi hali ni muhimu kuibua masuala yanayojitokeza ya jinsia - yakiwemo ubaguzi, unyanyasaji na mapengo ya jinsia katika kupata maendeleo na fursa. Haya yanakuwa ni sehemu ya makundi mahsusi kujadili na msingi wa kuweka vipaumbele vya jinsia katika Mpango wa Maendeleo wa Jamii, na katika mpango wa Halmashauri ya Wilaya.

Kuchambua kwa makini hali ya jinsia, wawezeshaji na Jamii ni lazima waelewe na kutambua kuwa jinsia ina sifa muhimu katika maendeleo. Wakati wa mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendelo ni vema kupata mawazo tofauti tofauti kutoka kwa makundi mbali mbali ya wanawake, wanaume, wavulana na wasichana pamoja na maskini pia makundi yasiyosaulika. Majadiliano na uchambuzi ni lazima uwezeshe Jamii kueleza kuchangamua kwa kudhamiria na kwa makini masuala ya jinsia wakati wa mchakato wa upangaji mipango shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.

Baada ya uchambuzi wa hali ya jinsia ni muhimu kuibua kuweka masuala ya mikakati juu ya jinsia) ambayo imeelezwa na Jamii. Mfano wa masuala ya jinsia yana weza kuwa ni;-

- Ukosefu wa maji safi na salama karibu na makazi
- Wasichana kuwa katika hatari ya kubakwa kwa kuwa njia inapitia shule iko katikati ya msitu mnene na vichaka.
- Ukosefu wa uwakilishi katika mfumo wa utoaji wa maamuzi
- Ukosefu wa usawa katika kumiliki rasilimali kti ya mwanamme na mwanamke.
- Ukiukwaji wa haki za binadamu kama wanawake kupigwa na ukeketaji.

Masuala ya jinsia yaliyotajwa yaliyojitokeza na Jamii ni lazima yaingizwe katika malengo ya mpango wao. Madhumuni au sababu za kuingiza masuala ya jinsia katika mpango wa Jamii ni ili kuhakikisha kuwa faida zitokazo na matokeo ya maendeleo zinanufaisha wanaume na wanawake kwa usawa.

Wakati mwingine inakuwa ni muhimu kuwa na malengo maalum kwa ajili ya wanaume au wanawake kwa kutegemea ni masuala gani yaliyojitokeza wakati wa kuchambua hali ya jinsia kwa mfano; masuala ya wanawake kukeketwa ambayo yanakiuka haki za wanawake au wasichana yanaweza yakahitaji kuwekewa lengo mahsusi katika mpango wa Jamii.

Pamoja na malengo maalum katika mpango ni lazima Jamii ibainishe mikakati na mbinu ambazo zitasaidia kushughulikia masuala ya jinsia. Ni vema pia kuonyesha katika mpango mgawanyo wa rasilimali za kutekeleza mikakati na mbinu zinazobainishwa katika mpango.

Mwishoni, ufuatiliaji na tathimini ni lazima upangwe na kufanyika ili kupima kwa kiasi gani msisimko/mwamko juu ya malengo yaliyowekwa yameweza kushughulikia masuala ya jinsia yaliyojitokeza katika Jamii. Kufikia hapa viashiria vya Jamii vya maendeleo na zana ya ufuatiliaji na tathimini zinahitajika ili kuleta mwamko wa jinsia pia zitasaidia kuleta usawa wa jinsia kwa wale wote watakaoshiriki katika ufuatiliaji na Tathimini shirikishi.

**Dhana muhimu za jinsia ni hizi zifuatazo**

***Jinsi***

Jinsi ni tofauti ya kimaumbile inayomtofautisha mwanaume na mwanamke. Maumbile hayawezi kubadilika katika hali ya kawaida. Kwa mfano maumbile ya kike au ya kiume yaani jinsi zao ndizo zinasababisha mtu aitwe mwanamke au mwanaume.

***Majukumu ya Jinsi***

Majukumu ya jinsi ni kazi za kibailojia au za kimaumbile. Kwa mfano kubeba mimba, kujifungua na kunyonyesha ni kazi za jinsi ya kike tu. Kazi za jinsi haziwezi kubadilika.

***Jinsia***

Neno hili linamaanisha ule mtazamo wa Jamii kwa mtu kuwa mwanamke au mwanaume. Ni mtizamo wa kijamii, kiutamaduni, na kisaikolojia kunakomtofautisha mwanamke na mwanaume katika Jamii. Kwa hiyo jinsia ni tafsiri ya Jamii.

***Mahusiano ya Kijinsia***

Dhana hii inaelezea jinsi mwanaume na mwanamke wanavyohusiana katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni katika Jamii yao Mahusiano haya ya kijinsia kwa kawaida hutokana na mchakato mzima wa malezi na makuzi na huimarishwa na mtu binafsi, familia, taasisi za kijamii, utamaduni na itikadi.

***Wajibu wa Kijinsia***

Hizi ni kazi mbalimbali, wajibu na matarajio ambayo Jamii imetafsiri na kupanga kufanywa na wanaume, wanawake, wasichana na wavulana. Kazi hizi sio lazima ziwe za kibailojia. Kwa hiyo zinaweza kubadilika kufutana na wakati na mazingira yaliyopo. Wajibu uliopangwa kufuatana na jinsi ni wajibu wa Jamii na umekuwa ukibadilikabadilika kutokana na wakati.

**Usawa wa kijinsia**

Dhana hii inaelezea utaratibu wa kutoa haki na fursa za maendeleo kwa watu wote bila kujali jinsi, umri au tabaka. Usawa katika haki na fursa za maendeleo hugusa michakato na Nyanja zote za maendeleo, kisiasa, kijamii, kisheria na kiuchumi.

**Ubaguzi wa kijinsia**

Ubaguzi wa kijinsia ni utaratibu wa kutoa mafao au haki kwa kufuata misingi ya jinsi. Utaratibu huu hudumishwa na mifumo inayojengwa katika Jamii nyingi na hivyo kupelekea ubaguzi dhidi ya wanawake katika mgawanyo wa mapato rasilimali na hata katika kutoa fursa za ushiriki katika maamuzi. Kwa mfano kumnyima mototo wa kike haki ya kurithi mali ya baba yake aliyefariki ni ubaguzi wa kijinsia.

**Pengo la kijinsia**

Pengo la kijinsia ni kipimo cha kutokuwepo usawa kijinsia. Pengo hili hudhihirika zaidi pale taarifa za takwimu zinapotolewa kwa mlinganisho kijinsia. Kwa mfano, takwimu za shule ya msingi ya Ero, Wilaya ya Arusha Vijijini za mwaka 1999 zilionyesha kuwa wavulana 90 kati ya 111 waliandikishwa darasa la kwanza ikilinganishwa na wasichana wote 105 waliofikia umri huo. Takwimu hizi zinaonyesha pengo la jinsia kwa tafsiri kuwa watoto wa kiume hawakuandikishwa wote shuleni

**Mwamko wa kijinsia**

Dhana hii inahusu kutambua kuwa wanawake na wanaume wana jukumu tofauti katika Jamii na kuwa mahitaji yao huwa tofauti na sharti yatambuliwe katika michakato ya maendeleo. Dhana hii pia inahusisha kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mipango katika mwamko wa kijijnsia

**Kuthamini jinsia**
Kutenda kwa haki; kutambua na kuthamini uwezo walionao wanawake na wanaume katika Jamii na Nyanja zote.

**Kutopendelea upande wowote kijinsia**
Kupanga kwa ajili ya wanawake, wanaume, wavulana, na wasichana bila kujali kuwa wako tofauti kaika mahitaji na majukumu. Kwa mfano kupanga bila kujali jinsia hakuoneshi hasa ni kwa vipi kutashughulikia mahitaji na masuala ya kijinsi. Mpango wa namna hii utazingatia Jamii kama Jamii tu, bila kujali tofauti za kijinsia zilizopo.

**Kujenga uwezo**
Ni mchakato ambao watu huchukua umiliki ili kukabili vikwazo. Kwa wanawake ni mchakato ambao wanawake huhamasisha ufahamu, uainishaji na kukabili unyanyasaji wa kijinsia ili kufikia usawa wa kijinsia.

**Haki sawa kijinsia**
Haki sawa na fursa kwa wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana katika Nyanja zote , kisiasa, kijamii, kisheria na kiuchumi.

**Kubainisha na kuainisha jinsia katika mchakato wa maendeleo**
Dhana hii inasisitiza kuwa jinsia ni suala muhimu katika maendeleo. Vilevile dhana hii inaelezea kuwepo kwa utaratibu wa kuingiza maswala ya jinsia katika mfumo na mchakato mzima wa maendeleo, hususani ile ya uandaaji sera na mipango. Kufanikiwa kubainisha na kuainisha jinsia katika mchakato wa maendeleo kutakuza usawa wa jinsia katika Jamii na kuhakikisha maendeleo endelevu.

***Jinsia katika mchakato wa upangaji mipango***

Zifuatazo ni hatua za kuingiza masuala ya jinsia wakati wa maadalizi ya mipango yenye msingi wa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo

1) <u>Elewa hali halisi ya Jamii</u>
Lengo ni kuhakikisha kuwa takwimu na taarifa zote zilizokusanywa zinaingizwa na kuchambuliwa kwa kina, katika msingi wa jinsia kwa kutumia uchambuzi wa pengo la kijinsia. Wakati wa mchakato wa kupanga masuala ya jinsia, lazima ukusanye makundi yote katika Jamii wakiwemo wanawake, wanaume, wavulana, wasichana na watoto.

2) Vipaumbele vya mahitaji ya kijinsia

Mahitaji yote ya kijinsia lazima yaingizwe katika mipango ya Jamii.

3) Kuweka malengo ya maendeleo.

Malengo ya maendeleo lazima yaweze kupimika na kuwa na msingi wa kijinsia. Kwa mfano kuongeza uandikishaji kutoka asilimia 50 kwa/ wavulana kwa asilimia 40 kwa wasichana kwa sasa hadi kufikia asilimia 90 kwa wasichana na wavulana wote waliofikia umri wa kwenda shule.

4) Kupanga mikakati.

Hizi ni juhudi za kuwa na mikakati itakayowezesha kufikia malengo ya maendeleo yaliyowekwa mathalani, kutokana na lengo la uandikishaji, mikakati inaweza kuhusisha uhamasishaji wa Jamii juu ya umuhimu wa elimu katika maisha hususan kwa wasichana. Aidha kujenga shule ndani ya Jamii yenyewe, ili kuboresha uandikishaji na kuwezesha uandandikishaji zaidi kwa wavulana na wasichana.

5) Utatuzi

Utatuzi utahusisha mabadiliko halisi ya mikakati kuwa vitendo halisi kwa mfano katika lengo la uandikishaji vitendo vitakuwa kuunda kamati ya shule yenye wajumbe mchanganyiko yaani wanawake na wanaume na kufanya zoezi la kuchambua kwa kina hali ya shule na mazingira yake kwa ujumla.

6) Tathmini

Utekelezaji wa mpango lazima upimwe kutokana na malengo ya maendeleo yaliyowekwa na sharti yazingatie jinsia.

### 3.3.2 Utawala Bora

Nchi yetu imekumbwa na shinikizo la rushwa, kutokuwajibika, mfumo wa sheria uliolemewa na unaoshindwa kufanya kazi vizuri na kutimiza haki za msingi za binadamu, na mmomonyoko wa maadili katika utendaji kazi wa sekta ya umma. Serikali imechukua hatua mbali mbali ili kushughulikia baadhi ya matatizo ya utawala sababu za kuwepo kwa matatizo haya ni nyingi lakini mojawapo ni ile ya kutokushirikisha Jamii kutoa maamuzi katika shughuli zao za maendeleo. Ndiyo maana Serikali imechukua hatua za makusudi za kuwawezesha wananchi kushiriki katika kuamua na kupanga juu ya maendeleo yao.

Kushirikisha Jamii kunaleta uwazi na uwajibikaji katika ngazi zote. Aidha ushiriki unaiwajibisha Serikali kuitikia matakwa ya wananchi badala ya Serikali kuifanyia Jamii maamuzi, kwa mfano katika ngazi ya Halmashauri ya Vijiji watu walio wengi hawahudhurii mikutano kwa sababu ya viongozi kutokuwa wa wazi kutowashirikisha wananchi katika kutoa maamuzi utekelezaji hafifu wa mipango ya maendeleo na matumizi mabaya ya fedha.

Utawala bora unachochea mabadiliko katika mitazamo mbali mbali ya Jamii na utawala wa sheria. Hii inaweza kufikiwa kwa kuijengea Jamii uwezo wa kufahamu haki zao za msingi ambazo zinachochea wajibu, uwazi na uwajibikaji. Hivyo basi Jamii lazima itumie haki yake ya msingi katika kufanya maamuzi ya maswala mbali mbali katika kujenga utamaduni wa ushirikiswaji kwa kupitia mikutano na kamati mbali mbali zilizopo Kijijini. Hii inahusisha kuzungumza wazi wazi na kutoa changamoto kwa viongozi wasiofaa na kuzingatia utawala wa kisheria kwa wote.

### 3.3.3 Haki za Binadamu

Haki za binadamu ni maadili ambayo lazima yakubalike na kila mtu. Haki za binadamu zimekuwa sehemu ya Jamii zote na zimekuwa zikibadilika na kukua kulingana na wakati. Haki hizi ndio msingi wa stahili na ulinzi katika maisha ya binadamu.

Sifa za haki za binadamu ni:

- *Hazigawanyiki*: Haki zote zinawahusu binadamu wote na hakuna haki inayoweza kusimama yenyewe.
- *Hutegemeana*: Haki zote hutegemeana. Kwa mfano, kuondoa haki ya kupata elimu, kutaathiri pia uhuru wa mtu kujieleza au kinyume chake.
- *Hazikiukwi*: Ni sehemu ya kila binadamu binafsi, hazikiukwi na wala hazihamishiki.

Kwa haki zote za binadamu, kuna mgawanyiko ufuatao;

- Mwenye stahili: Mtu ambaye ndiye au anaye stahili haki.
- Mwenye wajibu: Mtu au asasi ambayo ina wajibu wa kuhakikisha kuwa wadai/wastahili wanatimiziwa haki zao

Kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba yote ya haki za binadamu, Serikali ndiye muhusika mkuu mwenye wajibu. Wahusika wakuu wanawajibu wa;

- Kuheshimu haki za binadamu na kutokiuka kwa njia yeyote ile stahili ya haki.
- Kulinda haki za binadamu kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote anayekwenda kinyume na stahili ya haki.
- Kuwezesha haki za binadamu; kuweka mazingira ambayo yanaruhusu stahili ya haki na kutimiza haki za binadamu.
- Kutimiza haki za binadamu; kuchukua hatua zote zinazotakiwa kuhakikisha kuwa watu wote wanapata haki.

Hatua na vipengele muhimu katika kupanga mipango kwa mtazamo wa haki za binadamu,

**Uchambuzi wa Ukiukwaji**

Uchambuzi wa ukiukwaji unaanzia kwa upimaji ili kutambua ni haki zipi ama zimekiukwa au zimepuuzwa au ziko hatarini kukiukwa. Katika mchakato huu, upimaji ulenge katika kuyafichua makundi au watu binafsi katika Jamii ambao wanaathirika zaidi. Upimaji huu lazima pia uwe na mtazamo wa tatizo kama linavyojitokeza katika eneo fulani. Uchambuzi wa kiukwaji ni kuhusu kufanya upimaji wa matatizo yanayohusiana na ukiukwaji wa haki na sababisho.

Uchambuzi wa kiukwaji umepangwa katika mtiririko ili kuonesha ngazi za mahusiano kati ya sababisho za wazi na zile zilizofichika na ngazi za msingi. Ngazi ya kwanza ya ukiukwaji – sababu ya wazi – Inahusika moja kwa moja na mtu/watu binafsi, ambao ndio wanaodai haki mfano, asilimia 30 ya watoto ambao hawajaandikishwa shuleni ndio wanaodai haki. Sababisho la wazi la watoto haokutokuwepo shuleni linaweza kuwa wazazi wanawatumikisha watoto kusaidia shughuli za nyumbani, kama kulima, kufanya biashara ndogondogo au kulea watoto wachanga kama kwa mfano hatua zitachukuliwa tu katika ngazi ya mwanzoni, adhabu inaweza kutolewa kwa wazazi bila kutambua kwamba inawezekana kuwepo kwa sababisho zaidi katika ngazi nyingine.

***Mfano wa ukiukwaji wa haki ya mtoto***

Asilimia 30 ya watoto wenye umri wa kwenda shule katika Kijiji cha kona hawakuandikishwa shuleni. Watoto hawa hawapati haki yao ya msingi ya Elimu. Swali la kujiuliza hapa ni je kina nani wanaathirika zaidi kutokana na maumbile yao (wavulana au wasichana),miaka (7-13), kutoka kaya zipi? Kwa nini hawapo shuleni? Maswali kama haya yanatafuta kufanya uchambuzi wa sababisho zinazowazuia watoto wasifurahie haki yao ya kupata elimu. Hii inaelezea uchambuzi wa ukiukwaji.

Ngazi ya pili ya uchambuzi ni sababisho zilizofichika.

Hatua hii inaangalia sababu zinazohusiana na utaratibu wa utoaji huduma yakiwemo majengo, miundo mbinu na mifumo, kaya zinazohudumiwa na wenye stahili binafsi. Maeneo mbali mbali ya ukweli wa sababisho zilizofichika yanaeleza kwa nini asilimia 30 ya watoto hawako shuleni, kama vile;-

- Shule kuwa mbali sana na makazi ya watu.
- Michango mbali mbali ya shule inayopita uwezo wa wazazi wengi.
- Wazazi kutokuwa na taarifa kuwa elimu ni haki ya msingi ya binadamu kwa watoto wao.
- Mazingira duni ya shule yasiyovutia watoto, yaani shule iko ovyo ovyo

Kuchukua hatua katika ngazi ya sababisho zilizofichika ni muhimu, lakini haitoshi. Jambo la muhimu kabisa katika ngazi ya ukiukwaji ni sababisho za msingi. Ngazi hii inajishughulisha na msingi wa mambo muhimu ya kimfumo yanayohusu Jamii, uhumi, siasa na mfumo wa utamaduni.

Ukichukulia mfano wa aslilimia 30 ya watoto kutoandikishwa shuleni mambo mbalimbali ya msingi yanaweza kuelezewa kama sababisho nayo ni;-

- Umasikini; Wazazi wanashindwa kulipa michango ya shul vile vile baadhi ya watoto wanatumwa na wazazi wao kusaidia kufanya biashara ndogondogo ili kuongeza pato la familia.
- Mahusiano ya kijinsia: Watoto wa kike mara nyingi wanalazimishwa kubaki nyumbani kusaidia kulea watoto wachanga.
- Mgawanyo mbaya wa bajeti ya Elimu, shule inakuwa na hali duni isiyovutia watoto kuhudhuria shuleni.

Ikumbukwe kwamba uchambuzi wa ukiukwaji utatumika wakati wa mchakato wa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo hususan linapofanyika zoezi la kukusanya na kuchambua takwimu. Ni muhimu sana kutaja sababisho za mapengo ya maendeleo katika ngazi zote tatu. Msisitizo uwe katika ngazi ya msingi ya ukiukwaji. Matokeo ya uchambuzi huu yatasaidia kubainisha na kuweka malengo ya kurekebisha ukiukwaji wa haki za binadamu na hasa kwa wanawake na watoto.

**Uchambuzi wa Uwajibikaji**

- Kwa kila sababisho, yaani zile za wazi, zilizojificha na za msingi ni muhimu kuainisha nani anawajibika. Wale wenye wajibu ndio wanao wajibika kuhakikisha na kuwezesha upatikanaji wa haki.
- Ni muhimu kusisitiza kuwa mhusika mkuu katika upatikanaji wa haki za binadamu ni dola/ Serikali inaweza isiwe na uwezo wa kuhimiza haki zote lakini inatakiwa ihakikishe kuwa inaheshimu na kuwezesha haki kutendeka.
- Wengine wenye wajibu ni mtu mmoja mmoja; kaya , Jamii n.k. Wapo pia wengine amabo kwa sababu za kibinadamu huchukua wajibu kwa niaba ya wengine, wao hawawezi kuwajibishwa. Kwa mfano mama anayewapatia watoto wa nyumba ya jirani chakula mara kwa mara kwa sababu wazazi wao huweka mbele ulevi na hivyo kupuuza haki ya msingi ya watoto wao, anafanya hivyo kwa sababu za kibinadamu hawajibiki kufanya hivyo.
- Uchambuzi wa uwajibikaji unalenga katika kupata/kubainisha wahusika wakuu katika kutoa haki. Watu binafsi na Taasisi na uhusiano wao na wale (wastahili) ambao haki zao zimekiukwa kwa mfano;- Juma, ambaye ana umri wa miaka 9, na pia ni yatima hajaandikishwa shule. Juma anayo haki ya kuwa shuleni. Wale wenye wajibu wa kuhakikisha kuwa Juma anapata haki yake ya kuwa shuleni ni pamoja na Mjomba wake, shangazi, na bibi yake. Hawa ndiyo ndugu wa karibu ambao dai la haki ya Juma ya kuwa shuleni laweza kupelekwa.
- Kumbuka kuwa wale wadai wa haki wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa wanapata haki zao, hivyo basi ni muhimu kutambua kuwa mwajibikaji katika ngazi ya chini kama vile mzazi, pia ana haki ya kumuajibisha muajibikaji katika ngazi ya juu kama vile mamlaka ya ngazi ya Wilaya ; Idara za Serikali na wizara.
- Uchambuzi wa uwajibikaji katika mchakato wa upangaji wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo utahitaji kwamba wanaKijiji au Jamii viainishe wahusika wakuu ili hatua ziweze kuchukuliwa (ikiwa ni pamoja na kutoa haki) kwa jinsi inavyowezekana, uchambuzi lazima ushughulikie hatua zote kuanzia ngazi ya kaya hadi ya Taifa.

**Uchambuzi wa uwezo**

Swali muhimu la kujiuliza katika hatua hii ni: Kwa nini wahusika wakuu hawatekelezi wajibu wao? Katika mchakato wa upangaji mipango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo wahusika wakuu wanaoangaliwa ni taasisi kama vile Halmashauri ya Kijiji, kamati mbali mbali wazazi, walimu, Jamii wataalamu katika ngazi zote n.k. Ni muhimu kupima na kuchambua ni kwa kiasi gani wale walioainishwa kama wahusika wakuu wana uwezo wa kutimiza majukumu yao.

Uwezo wa kupanga kwa mtazamo wa haki za binadamu umetafsiriwa kwa upana sasa kuliko ilivyokuwa awali. Katika dhana ya upangaji kwa mtazamo wa haki za binadamu, uchambuzi wa uwezo unaangalia kama mhusika mkuu anazo hisia za uwajibikaji, kujituma, motisha na rasilimali kutekeleza mjukumu. Rasilimali hapa inamaanisha ufahamu, ujuzi, kuwa na taarifa, vifaa kwa utaratibu. Mambo mengine ni uwezo wa usimamizi, na uwajibikaji.

Uchambuzi wa uwezo unasaidia kuainisha mapengo ya uwezo ambayo yanahitaji utatuzi ili kuhimiza maendeleo ya Jamii na kutekeleza haki za binadamu. Hii ni sehemu muhimu katika mchakato wa upangaji wa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo kuhakikisha kuwa ufumbuzi uliopangwa unaelekezwa kwa wale waliopewa jukumu la kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinafurahiwa na kila mtu katika Jamii hasa wanawake, watoto na makusudi yaliyosahaulika.

**Kanuni Muhimu za haki za binadamu za Kuangalia Wakati wa Mchakato wa Upangaji wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.**

Upangaji mipango kwa mtazamo wa haki za binadamu unamaanisha kufanya mchango muhimu katika kutambua haki za binadamu na kuishi kwa kufuata kanuni za haki za binadamu. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inatamka malengo ambayo yanaweka msingi wa haki za binadamu kwa watanzania kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kisiasa. Mtazamo wa haki za binadamu katika kupanga ni mchakato na matokeo. Huwezi kuwa na mpango wa haki za binadamu ulioandaliwa kwa namna ambayo ni kinyume na kanuni za haki za binadamu.

Upangaji Mipango kwa Mfumo wa Fursa na Vikwazo lazima Uongozwe na Kanuni za Haki za Binadamu Zifuatazo:

**<u>Ushirikishwaji</u>**

Hii ni dhahiri katika mchakato wa upangaji kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Ni vema kuhakikisha kuwa makundi yote katika Jamii yanashiriki ipasavyo vinginevyo inawezekana mpango wa Jamii ambao unawakilisha maoni ya watu wachache tu katika Jamii (kama vile matajiri tu na wazee). Mjadala mkubwa uliokuwepo miaka michache iliyopita ulikuwa juu ya ushiriki wa wanawake. Sasa hivi ni muhimu kutambua umuhimu wa kuwashirikisha wanawake, vijana na watoto wa jinsia zote katika mchakato wa upangaji wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Ufanisi katika kupanga kwa kutumia makundi ni vema uruhusu uundaji wa makundi ya vijana wa kike peke yao, na wakiume peke yao. Kuwaingiza vijana katika makundi ya wazee kunaweza kusababisha sauti zao zisisikike.

Ikumbukwe kuwa ushirikishwaji lazima uwe kulingana na umri na uwezo wa kufikiri pia kwa mfano watoto wa umri wa miaka tisa na kuendelea wanaweza kueleza mawazo yao juu ya mambo ambayo yanawahusu wao.

### 3.3.4 UKIMWI

Janga la UKIMWI linarudisha nyuma maendeleo ambayo yamekwisha patikana kwa Watanzania katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Takwimu zinaonyesha upungufu mkubwa wa nguvu kazi unaondelea kutokea katika sehemu za kazi hivyo kuathiri mfumo mzima wa utoaji huduma kwa wananchi. UKIMWI umeathiri kwa kiasi kukubwa uwezo wa kaya na Jamii kujikimu kutokana na kuugua au kufariki kwa wazazi na kuacha watoto katika maisha magumu na kuongeza mzigo kwa ndugu na Jamii kwa ujumla. Ni muhimu basi kuhakikisha kuwa mipango yote ya maendeleo katika ngazi zote inatiliwa maanani suala la UKIMWI. Ni muhimu kuhakikisaha kuwa utaratibu mzima wa kuibua fursa, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo, unazingatia athari za UKIMWI katika kufanikisha malengo yaliyopangwa.

**UKIMWI** ni upungufu wa kinga mwilini. Virusi vya UKIMWI ni viini vinavyoshambulia kinga ya mwili ya kupigana na magonjwa. Virusi vya UKIMWI hushambulia na kuharibu uwezo wa mwili kujikinga na magonjwa. Watu wenye UKIMWI hufa kutokana na miili yao kushidwa kupigana/ kustahimili mashambulizi ya magonjwa kama kifua kikuu, kuharisha na malaria na mengineyo. UKIMWI hauna tiba wala chanjo.

**Njia za maambukizi ya UKIMWI**

Njia kuu ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI ni ngono isiyo salama ambayo inachangia kwa asilimia 90 ya maambukizo yote. Njia nyingine za maambukizo ni kuwekewa damu yenye virusi vya UKIMWI, kushirikiana kutumia vifaa mbalimbali vinavyoweza kutoboa ngozi na kuingia kwenye damu mfano; nyembe, vifaa vya kutogea, kukeketa na kutahiria; pamoja na kutoka kwa mama mwenye virusi vya UKIMWI kwenda kwa mtoto wakati wa mimba, wakati wa kuzaa na wakati wa kunyonyesha.

**Dalili za maambukizi ya UKIMWI**

- Kupotewa na nguvu mwilini ambako hakuna sababu za waziwazi.
- Kupoteza uzito kiasi cha asilimia 10 kwa muda mfupi.
- Kuharisha kwa muda wa mwezi mmoja na zaidi.
- Homa za mara kwa mara na za muda mrefu.
- Kuvimba tezi hasa za shingo na makwapa.
- Kupumua kwa taabu na kikohozi kikavu na vichomi.
- Utando mweupe na vidonda mdomoni kinywani na kooni (maumivu kooni wakati wa kumeza chochote).
- Kuchanganyikiwa kwa kutokana na madhara katika ubongo na ngozi inayozunguka ubongo na uti wa mgongo.
- Vidonda katika sehemu za siri.
- Ukurutu au upele unaowasha.
- Kupungukiwa damu mwilini
- Kansa ya ngozi.

**Hali ya Maambukizo**

Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2000 makisio kutoka Mpango wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI yanaonyesha kuwa idadi ya waliokuwa na UKIMWI ni zaidi ya 700,000 na wale ambao wanaishi na virusi ni 2,000,000. Asilimia 70.5 ya maambukizo ni kwa watu wenye umri kati ya miaka 25 hadi 49. Asilimia 15 ni wale wenye umri wa miaka 15 – 24. Wanawake wanaambukizwa katika umri mdogo zaidi. Kati ya maambukizo mapya asilimia 69 ilikuwa ni ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 na 24. Wakati huo huo zaidi ya watoto wachanga 70,000 waliambukizwa. Takwimu za Kitaifa zilizokusanywa kati ya mwaka 2003 na 2004 Tanzania Bara zinaonyesha kuwa asilimia 7 ya watu wazima (umri wa miaka 25 – 49) wameambukizwa virusi vya UKIMWI. Pia, takwimu zinaonyesha kuwa, kiwango cha maambukizo ni kikubwa zaidi kwa wanawake (asilimia 8) kuliko wanaume (asilimia 6)

## Sababu za Maambukizo ya UKIMWI

Sababu kubwa zinazosababisha maambukizi ya UKIMWI ni pamoja na umasikini, ujinga, ukosefu wa vifaa vya kujikinga, ukosefu wa taarifa muhimu kuhusu UKIMWI, kutoshirikisha Jamii hasa vijana katika kupanga mikakati ya kupambana na UKIMWI, ukosefu wa huduma rafiki za afya zinazowajali vijana (Youth friendly health services) n.k.

*Ukosefu wa taarifa muhimu kuhusu UKIMWI*

Japo watu wengi wanafahamu madhara ya UKIMWI, uelewa huu bado ni wa juu juu tu. Kwa mfano, katika matumizi ya Kondomu watu wengi hukutumia kondomu wakati mahusiano yanapoanza. Baada ya muda kupita, uhusiano wao unapoendelea wengi huacha kutumia Kondomu. Hii inaonyeasha uelewa hafifu kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

*Kutoshirikishwa kwa watoto na vijana*

Katika kupanga mikakati ya kupambana na UKIMWI katika ngazi mbalimbali watoto na vijana mara nyingi hawashrikishwi. Badala yake hutakiwa kufanya vitu ambavyo hawavielewi undani wake na matokeo yake ni kwamba wengi hawafuati kwa vile hawaelewi umuhimu wake. Sehemu ambazo watoto na vijana wamehusishwa katika kupanga mikakati ya kupambana na UKIMWI, wengi wameonyesha upeo mkubwa wa kuelewa na ari kubwa ya kutekeleza.

*Ukosefu wa ajira*

Katika ngazi ya kaya wazazi wengi huwawia vigumu kuwapatia watoto wao ardhi au rasilimali nyingine ili waweze kujikimu. Matokeo ni kwamba vijana wengi hawana cha kufanya na kwa wavulana wengi wanakuwa katika hatari ya kujiingiza katika vitendo vibaya ikiwa ni pamoja na kujiingiza kwenye vitendo vya zinaa na ubakaji wasichana .a utumiaji wa madawa ya kulevya. Kwa upande wa wasichana wengi wao hukosa ajira na huishia kufanya kazi za ndani na wegine hujiingiza kwenya shughuli za kuuza miili yao ili kupata fedha za kujikimu.
Mambo yote haya huchangia katika kuenea kwa UKIMWI.

*Ukosefu wa ushauri, vifaa vya kujikinga na huduma rafiki*

Katika sehemu nyingi, hasa Vijijini, hakuna huduma za uhakika zinazohusiana na kujikinga na maambukizo ya magonjwa ya zinaa na hasa UKIMWI. Vijana wengi wakiambukizwa ugojwa wa zinaa hushindwa kwenda zahanati kwa kuhofia kusimangwa au kusemwa na Jamii. Matokeo yake wengi huamua kujitibu kwa njia za kienyeji ambazo si za uhakika. Katika sehemu zingine imegundulika kuwa baadhi ya vijana wanatumia mifuko ya plastiki kama kondomu! Hii inaonyesha dhahiri matatizo katika upatikanaji wa kondomu na vilevile uelewa hafifu kuhusu jinsi ya kujikinga na maambukizo ya UKIMWI.

**Athari za UKIMWI**

Athari za UKIMWI zinaweza kuonekana au kujitokeza katika maeneo yafuatayo:-

*Watoto yatima*

Idadi ya watoto yatima Tanzania ni kubwa na inazidi kuongezeka. Kwa mujibu wa takwimu za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) hadi mwisho wa mwaka 2000 ilitarajiwa kuwa idadi ya watoto yatima kutokana na UKIMWI ingefikia watoto 800,000. Watoto yatima mara nyingi hupoteza haki zao kwa kukosa matunzo, elimu na hata lishe bora. Wengi wao huacha shule na kuingia kwenya ajira za watoto ili kujikimu kimaisha. Wengine huajiriwa kama wafanyakazi wa ndani ambako hupata mateso mengi ikiwa ni pamoja na kunyanyaswa na kubakwa. Wengine huishia kuwa watoto wa Mitaani.

*Kupungua kwa nguvu kazi*

Kundi la vijana ndilo liko hatarini zaidi. Vijana wengi hujihusisha na ngono mara tu baada ya kupata balehe /kuvunja ungo na wengi hawatumii kinga zozote. Asilimia 60 ya maambukizo mapya hutokea kwa vijana wenya umri kati ya miaka 15-25 hasa wasichana.

*Kutengwa na Jamii*

Mara nyingi waathirika wa UKIMWI na familia zao hutengwa na Jamii *(unyanyapaa).* Watoto ambao wazazi wao wamefariki kwa UKIMWI mara nyingi wanabaguliwa; katika maeneo mengine wanawake waliofiwa na waume zao hutengwa na Jamii

**Athari nyingine za UKIMWI ni pamoja na hizi zifuatazo:**

- Kupoteza rasilimali za kaya
- Kupoteza muda wa kazi kwa kuumwa au kuuguza mgonjwa
- Kupungua kwa tija
- Kuongezeka kwa gharama za matibabu
- Kuongezeka Bima na gharama zingine za kinga ya Jamii
- Kuongezeka kwa gharama za mazishi
- Kuongezeka familia tegemezi
- Kuoengezeka kukiukwa kwa haki za wanawake na watoto.

**Njia za Kujikinga na Maambukizo ya UKIMWI**

Kazi kubwa inaendelea kufanywa na wataalamu usiku na mchana kutafuta dawa au chanjo ya UKIMWI, lakini mafankio bado hayajafikiwa. Hata hivyo inawezekana kupunguza uwezekano wa kuambukizwa na ugonjwa huu kwa kuzingatia yafuatayo.

**Kuwa na Mpenzi mmoja:** Kuacha kufanya mapenzi ya ovyo na kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu.

**Kutumia Kondomu:** Matumizi ya mpira wa kuvisha uume (kondomu) pamoja na matumizi ya kondomu za kike yanaweza kupunguza hatari ya kuambukizwa. Hata hivyo matumizi ya njia hizi yanahitaji uangalifu mkubwa kuzuia uwezekano wa mipira kupasuka kwa kutumia vibaya. Matumizi ya kondomu basi, yanahitaji maelekezo sahihi.

**Kuepuka kushirikiana miswaki, nyembe, vifaa vya kutogea masikio na pua**, vifaa vya kutahiri na kadhalika, ambavyo havikuchemshwa vya kutosha. Vile vile kuhakikisha kuwa sindano na vifaa vingine vinavyohusika na wagonjwa hospitalini, kama inabidi visitumike zaidi ya mara moja, na pale inapobidi vitumike zaidi ya mara moja basi vifanywe salama vya kutosha kwa kuchemsha au kutumia joto kali kabla havijatumiwa na mtu mwingine.

**Kuachana na utumiaji wa madawa ya kulevya** hasa utumiaji wa kujidunga sindano na kushirikiana na matumizi ya sindano ambayo huelekea kuleta maambukizi ya UKIMWI na hatimaye kupanua eneo la hatari kwa kuongeza watu wenye ugonjwa huu katika Jamii.

**Wanawake** walioambukizwa UKIMWI waepuke kubeba mimba, maana watoto watakaowazaa wanaweza kuzaliwa na ugonjwa huu, au kuupata muda mfupi tu baada ya kuzaliwa hasa kwa njia ya kunyonya maziwa ya mama.

### 3.3.5 Menejimenti ya Mazingira

**Maana ya mazingira**

Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavomzunguka binadamu mahali anapoishi kama vile udongo, hewa, maji, wanyama pori, na misitu.Kuwepo maendeleo endelevu ni pamoja na kuwepo usafi wa mazingira na hifadhi ya mazingira. Dhana hii inahusisha kuwepo uwiano kati ya nyanja za maendeleo, desturi, mahitaji muhimu na utunzaji wa mali asili kwa matumizi ya kizazi kilichopo na kizazi kijacho.

*Menejimenti ya mazingira*

Mazingira yana viumbe mbalimbali vinavyomzunguka binadamu. Katika mzunguko wa maisha ya viumbe hai, viumbe vyote hai na visivyo hai vinategemeana. Ukiondoa kimojawapo, viumbe vingine vinaathirika. Kwa msingi huo inabidi kuwepo menejimenti ya mazingira.

*Sababu za kufanya menejimenti ya mazingira*

Menejimenti ya mazingira hufanywa kama hatua madhubuti za kuzuia/ kuthibiti athari na majanga yanayoweza kusababishwa na uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Athari na majanga hayo ni kama ifuatavyo:

*Athari*

- Kutokea kwa jangwa (ardhi kubaki wazi, kupotea kwa uoto na wanyama, kubadilika kwa hali ya hewa na kuleta ukame na uhaba wa mvua)
- Mmomonyoko wa udongo
- Kuingia mchanga tope kwenye mabwawa, maziwa na mito unao hatarisha viumbe wa majini
- Uchafu na kuharibika kwa usalama wa maji unasabisha milipuko ya magonjwa kama kipindupindu, kuharisha damu n.k.
- Kupotea kwa bioanuai hususan udongo na uoto kutokana na kukusekana kwa chakula chake.
- Uchafu wa hewa unasababisha magonjwa kama vile Saratani, Kipindupindu, Homa za matumbo n.k.

**Majanga**

- Kimbunga
- Upepo mkali
- Maporomoko ya ardhi
- Mafuriko
- Ukame
- Mlipuko ya magonjwa mbalimbali

**Mipango ya kudhibiti uharibifu na uchafuzi wa mazingira**

Hii ni zana kubwa ya menejimenti ya mazingira. Vijiji na ngazi nyingine inabidi wa wianishe mipango yao ya maendeleo na mipango ya kudhibiti uharibifu na uchafuzi wa mazingira ili kuwa na mipango yenye misingi ya maendeleo endelevu.

Kazi za kufanya ili kuhifadhi mazingira ni kama ifuatavyo:

## Udongo

- Kilimo mseto
- Kurutubisha ardhi
- Kufuga kulingana na ukubwa wa eneo la malisho
- Kuweka makinga maji katika mashamba yaliyoko kwenye mwinuko
- Kutolima kwenye miteremko mikali
- Kufunika ardhi kwa kutumia masalia ya mimea

## Hewa

- Kupunguza mitambo na vitu vingine vinavyochafua hewa
- Kuharibu na kuteketeza madawa na taka za sumu kwa uangalifu

## Maji

- Kuzuia kuwepo makazi wala kufanya shughuli za kiuchumi karibu na vyanzo vya maji
- Kuzuia utupaji taka kwenye mito, maziwa, mabwawa na bahari
- Kupanda miti inayohifadhi maji
- Kudhibiti mchanga tope unaoingia katika mito, maziwa na mabwawa

## Wanayama pori/ wanyama wa majini

- Kudhibiti uwindaji na uvuvi haramu
- Kutenga na kuhifadhi mbuga na mapori ya wanyama

## Misitu

- Kudhibiti uvunaji holela wa mazao ya misitu
- Kuzuia uchomaji moto misitu
- Kupanda miti
- Kutenga na kutunza misitu ya hifadhi
- Kuendeleza nishati mbadala kupunguza matumizi ya kuni na mkaa

### 3.3.6 Maafa

Maafa ni matukio makubwa ya hatari ambayo yanaharibu utaratibu wa maisha ya Jamii na hivyo kusababisha madhara yanayopita uwezo wa kuyakabili kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Kutokea kwa maafa kunaweza kuwa kwa haraka au polepole kutegemeana na mwendo kasi na muda tangu kuanza kwake kutokea na madhara yake. Maafa ya kiasili na yale yanayosababishwa na binadamu, yote yanaweza kuwa ya pole pole au ya haraka.

**Aina za Maafa**

Maafa yanaweza kugawanywa katika makundi matatu kama ifuatavyo:-

- Maafa ya Kiasili
- Maafa yanayosababishwa na binadamu
- Maafa yaletwayo na mchanganyiko mbali mbali wa madhara.

**Maafa ya Kiasili**

Maafa ya aina hii hutokea katika sura mbili, sura ya kwanza ni yale yanayodumu kwa muda mrefu kwa mfano ukame, njaa, magonjwa na uharibifu wa mazingira. Sura ya pili ni yale yanayodumu kwa muda mfupi kwa mfano tetemeko, maporomoko, upepo mkali, mafuriko, kimbunga na milipuko ya volcano.

**Maafa yanayosababishwa na Binadamu**

Haya ni maafa yanayosababishwa na vichocheo vya binadamu baadhi ya mifano halisi ni kama kudidimia au kubomoka kwa bwawa la maji kwa sababu ya ujenzi usio kuwa makini, au michoro iliyokosewa, uwashaji moto ovyo, ulipuaji mabomu, ugaidi, ajali za viwandani kama vile viwanda vya kemikali, mitambo ya mafuta, mitambo ya nyukilia na mabomba ya mafuta. Ajali zinazohusisha magari, ndege, magari moshi, meli na machafuko ya kisiasa.

**Maafa yaletwayo na mchanganyiko wa sababu mbali mbali**

Haya ni maafa yatokanayo na mlolongo wa maafa kwa mfano migongano na vita vya muda mrefu ambayo yanasababisha maafa mengine kama njaa, milipuko ya magonjwa wakimbizi n.k.

**Sababu za maafa**

Umaskini:

Umaskini ni mojawapo ya sababu kubwa zinazochangia kuwepo kwa maafa, hasa yale yanayosababishwa na binadamu. Watu fukara walio kosa elimu, mara nyingi hukosa mbinu na uwezo wa kuweza kukabiliana na kuyamudu mazingira yao. Kwa mfano kujenga nyumba kiholela, matumizi mabaya ya ardhi na uchafuzi wa mazingira.

Ongezeko la watu lisilodhibitiwa

Ongezeko la watu lisilodhibitiwa linaweza kusababisha kuwepo kwa hatari katika makazi kama vile magonjwa, upungufu wa rasilimali na migongano/mifarakano ya kijamii.

Ukuaji wa haraka wa Miji na Uhamiaji

Ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohamia mjini bila utaratibu muafaka unasababisha ukosefu wa maeneo salama kwa ajili ya ujenzi wa makazi na upungufu mkubwa wa rasilimali. Matokeo ya ukuaji haraka wa miji husababisha maafa yanayosababishwa na binadamu. Maafa mengi ya mafuriko mijini yanayohusishwa na kutodhibiti ukuaji wa miji unaosababishwa na watu wenye kipato duni kuishi kando kando ya mito na mabonde na kusababisha mafuriko.

Uharibifu wa Mazingira

Maafa mengi husababishwa au kuongewa makali na uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, ukataji wa miti ovyo husababisha mmomonyoko wa udongo na kuleta mafuriko na upungufu wa mvua. Uharibifu wa mikoko kando kando ya bahari au sehemu za maji maji (kinamasi) pwani hupunguza uwezo wa kuzuia upepo mkali wa msimu na vimbunga na hivyo kuleta maafa.

Ukosefu wa taarifa na ulelewa mdogo

Maafa pia yanaweza kutokea kwa sababu watu maskini amabo wamesahaulika kwa kukosa elimu ya kuepukana na madhara au kuchukua hatua za kukabiliana matukio ya maafa. Wakati mwingine sio lazima iwe ni ujinga ukosefu wa elimu tu bali pia ukosefu wa ufahamu wa hatua zipi zichukuliwe ili kujenga majengo imara na katika maeneo salama. Wengine wanakosa uelewa wa jinsi ya kupata msaada wakati wanapopata madhara makubwa.

Vita na migongano ya Jamii

Vita na migongano ya Jamii ni mojawapo ya matukio yanayoweza kusababisha maafa. Vita na migongano ya kijamii mara nyingi inaweza kusababisha watu kuhama makazi sababisho kubwa la vita na migongano ni pamoja kinyanganyiro cha rasilimali chache zilizopo, migongano ya dini na tofauti za kiitikadi.

Kukabiliana na mafaa

Kukabiliana na maafa ni msamiati mpana- unaotumika kuelezea shughuli zote zinazohusiana na kupunguza uharibifu utetwao na maafa. Shughuli hizi zinahusisha zile za kabla na baada ya maafa. Hivyo basi kukabiliana na maafa ni mchanganyiko wa shughuli nyingi zinazohusiana na sio mfululizo wa matukio ambayo yanaanza na kusimama kila baada ya tukio la maafa.

**Menejimenti ya maafa**

Vipo vipengele vitatu ni muhimu katika kukabiliana na Maafa.

- Kujiandaa kukabiliana na maafa.
- Kukabili maafa.
- Kuzuia maafa.

Kukabiliana na maafa kuna malengo makuu matatu kama ifuatavyo:-

- Kupunguza au (kuzuia kama inawezekana) uharibifu mkubwa utokanao na mwingiliano kati ya madhara na watu walio katika hatari kubwa kuathirika.
- Kuhakikisha msaada wa haraka na muafaka kwa watu walioathirika na maafa.
- Kufikia kwa haraka urejeshwaji endelevu wa hali ya kawaida.

Uzoefu wa Maafa yaliyowahi kutokea Tanzania.

- Ajali kubwa za vyombo vya usafiri
- Magomvi/Migogoro ya kutokuelewana ndani na nje
- Vimbunga na upepo mkali
- Ukame
- Matetemeko ya Ardhi
- Milipuko ya magonjwa
- Moto
- Mafuriko
- Maporomoko ya ardhi
- Wanyama waharibifu; ndege na wadudu
- Wakimbizi
- Maafa yatokanayo na Teknolojia.
- Milipuko ya volcano.

## 3.4 Maandalizi ya Kijamii

Kama ilivyokwishagusiwa mwanzoni, mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni mchakato shirikishi, ambao umeandaliwa kuiwezesha Jamii kumiliki agenda ya maendeleo yao. Hata hivyo dhana hii mpya inaweza isieleweke na kukubalika kwa urahisi kama watekelezaji hawatakuwa wameandaliwa vya kutosha kuipokea. Kwa hiyo, maandalizi ya Jamii ni mchakato wa kujenga uelewa juu ya umuhimu wa upangaji mipango shirikishi kwa ajili ya ufanisi wa utendaji kwa wahusika wote. Inahusisha uhamasishaji wa watekelezaji ili kuelewa wajibu na majukumu yao. Vilevile inatia chachu na kuamsha ari miongoni mwa watekelezaji ili kushiriki katika mchakato wa kuandaa na kuteleza mipango yao. Kwa mtazamo huu, maandalizi ya Jamii ni kigezo muhimu kwa ajili ya uendelevu wa mchakato.

*<u>Umuhimu wa Maandalizi ya Kijamii katika ngazi mbalimbali</u>*

Maandalizi ya Jamii yanahitajika katika ngazi mbali mbali, ikiwa ni pamoja na ngazi za maamuzi na utawala, na katika ngazi ya Jamii pia. Maandalizi ya Jamii ni muhimu kwa ajili ya kujenga mazingira ya Jamii kuuelewa na kuupokea vizuri mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Hii itawezesha kujenga umiliki kuanzia kupanga hadi utekelezaji wa mipango. Hata hivyo, uelewa wa Jamii pekee hautakuwa na maana kama vipaumbele vilivyoainishwa katika mipango havitaheshimiwa na mamlaka husika, katika ngazi za mamlaka ya Serikali za Mitaa na Serikali kuu.

Kwa lugha nyepesi, mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo unaweza kuangaliwa na Jamii kama ni muhimu pale ambapo watu watakuwa na uhakika kwamba watoa maamuzi na viongozi katika ngazi mbali mbali za Serikali wana uelewa sawa kuhusu mchakato na hivyo watasaidia. Ikiwa mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo utapewa uzito sawa na watendaji wote, mpango hautaonekana na Jamii kama utaratibu tu bali ni hatua halisi na muhimu katika kubadilisha maisha yao,na kufikia azma ya Serikali ya kurudisha madaraka zaidi kwa umma. Hali hii itawezesha Jamii kumiliki agenda ya maendeleo kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa mipango yao ya maendeleo.

*Ngazi za Utoaji maamuzi na Utawala*

Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa mamlaka ya kisheria ya kupeleka madaraka kwa watu, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mchakato wa upangaji mipango kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni hatua ya kuelekea kufikia mlengo makuu ya kutoa madaraka kamili kwa watu. Hatua hii inawawezesha watu kushiriki katika kupanga na kutekeleza mipango katika ngazi ya Jamii. Hata hivyo, umaana wa upangaji mipango shirikishi kama kipengele muhimu cha kupeleka madaraka na mamlaka kwa Jamii lazima kieleweke na kuzoeleka na watekelezaji wote katika ngazi za halmashauri na Serikali kuu. Uelewa wa mipango shirikishi utaboresha maudhui ya upangaji na bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vya Jamii na muda muafaka wa kutekeleza shughuli. Kwa mtazamo huu, maandalizi ya kijamii yanahitaji kuanzia katika ngazi za juu ili kujenga hali ya kujituma katika mchakato wa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na kuwawezesha wafanya maamuzi kuunga mkono mchakato wa upangaji mipango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na kupeleka rasilimali kwa ajili utekelezaji wa mipango ya Jamii kadri itakavyoonekana inafaa [2].

***Maandalizi ya kijamii katika ngazi ya utawala na utoaji maamuzi***

**Lengo:** Kutoa mafunzo ya uelewa kwa viongozi na watendaji wakuu wa Serikali juu ya mchakato wa kupanga mipango shirikishi kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Hii ina maana kwamba, viongozi na watendaji hawa watapata uelewa na kuona umuhimu wa mipango ya Jamii na hatimaye kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.

**Dhana:** Mamlaka katika ngazi mbalimbali zitafanya maamuzi baada ya kupata uelewa wa kutosha. Bila kuwa na uelewa wa kutosha ni dhahiri kuwa zitafifiza jitihada za Jamii. Zaidi ya hayo, Jamii ikitambua kuwa inaungwa mkono na mamlaka zinazohusika itatoa ushirikiano wa kutosha katika kufikia malengo waliyojiwekea.

Mafunzo ya uelewa yanashirikisha watendaji wa Serikali wafuatao:

[2] Ieleweke kuwa, katika kutekeleza mipango, Jamii inafanya tu yale yaliyo ndani ya uwezo wake. Kwa mfano, Jamii inaweza kuwa na mpango wa kupunguza vifo vya watoto wachanga ikiwa ndiyo kipaumbele chao, na hatua ya utekelezaji ya kujenga Zahanati. Katika hatua hii wanaKijiji wanaweza kujenga jengo la zahanati. Lakini jengo la zahanati tu halitoshi mpaka mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya afya wawezeshe upatikanaji wavifaa na watumishi wa afya.

*Makatibu wakuu wa Wizara*

Watendaji hawa wana jukumu kubwa la kuandaa sera mbalimbali za Taifa zinazohusiana na Wizara zao na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa. Uelewa na uwajibikaji wao katika mchakato wa upangaji mipango shirikishi ni muhimu hususani katika kuratibu sera hizo sambamba na mahitaji ya Jamii. Kwa kuwa mahitaji ya Jamii yanapatikana kupitia Wizara na sekta zaidi ya moja ni muhimu wafanya maamuzi katika Wizara na sekta hizo, kuwa na uelewa wa kutosha katika suala zima la mipango shirikishi.[3]

*Makatibu Tawala wa Mikoa*

Makatibu tawala mikoa wanatarajiwa kutoa ushauri katika mipango ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo kwa ujumla inatokana na mipango ya Jamii. Ili kufikia azma hii hapana budi watendaji kuulewa barabara mchakato wa upangaji mipango shirikishi kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.

## ***Maandalizi ya kijamii katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa***

**Lengo:** Kufanya mafunzo ya uelewa katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa juu ya mipango shirikishi na kuwezesha uratibu wenye ufanisi katika kutekeleza mipango ya Jamii.

**Dhana:** Viongozi na watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ndiyo wanaofanya kazi na Jamii katika mchakato mzima wa kupanga na kutekeleza mipango. Endapo watakuwa hawana uelewa wa kina juu ya mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo itakuwa vigumu kwao kuifikisha Jamii katika dhamira yake.

*Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji na Maafisa mipango/ wachumi.*

Uelewa wa kina juu ya mipango shirikishi Jamii kwa watendaji hawa ni muhimu sana kwa sababu wao ndio waratibu wakuu wa upangaji mipango shirikishi katika halmashauri zao. Zaidi ya hayo, wanapewa mamlaka haya kutokana na sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na.7 – 10 ya mwaka 1982 na ibara ya 145 na 146 za katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinazotaja hatua zinazolenga kutoa madaraka zaidi kwa umma katika kutoa maamuzi juu ya mipango ya maendeleo yao. Pamoja na haya, watendaji wa halmashauri wakipata uelewa wa kutosha watatenda haki na kutumia vizuri madaraka waliyopewa katika kuwezesha Jamii kutakeleza mipango yao. Ikumbukwe pia mipango ya mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa sehemu kubwa inatokana na mipango ya Jamii.

[3] Kwa kuwa mahitaji ya Jamii yanapatikana kutokana na mipango ya uwiano hivyo uratibu ni muhimu katika utekelezaji wa mipango hiyo ili kuepuka matumizi mabaya ya rasilimali. Mfano suala la kupunguza vifo vya uzazi litahusisha hatua za sekta ya afya, elimu, kilimo, miundombinu n.k. ili kufikia lengo lililotarajiwa.

### ***Kujenga uwezo kama sehemu ya maandalizi ya kijami***

**Lengo:** Kujenga uwezo wa wataalamu wa OWM-TAMISEMI na wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuratibu upangaji mipango shirikishi Jamii kwa ufanisi.

**Dhana:** Kujenga uwezo juu ya upangaji mipango shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo kwa wataalamu na watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni muhimu kwa ajili ya uratibu na uwezeshaji wa zoezi.

*Wataalam OWM-TAMISEMI*

OWM-TAMISEMI ndiyo mratibu mkuu wa upangaji mipango shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Wataalamu chini ya uratibu wa Wizara wanastahili kuelewa barabara yaliyomo katika maboresho yanayoendelea sasa hususani kurudisha madaraka kwa Umma na maudhui ya mipango shirikishi. Ili kufikia azma hii ya Serikali, ni muhimu kuwashirikisha katika mafunzo ya mipango shirikishi Kwa kuwajengea uwezo zaidi. Pia ni muhimu kuwapeleka katika nchi nyingine ambazo zinatumia mbinu ya mipango shirikishi kwa lengo la kuwapa uzoefu.

*Wataalamu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.*

Hawa ndio waratibu na wawezeshaji wa mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Wana jukumu la kuwezesha Jamii wakati wa kuandaa na kutekeleza mipango yao. Kuwajengea uwezo ni muhimu ili waweze kuelewa maudhui ya mchakato wa upangaji mipango shirikishi na hatimaye kuwa na uwezo wa kuratibu na kuwezesha Jamii kwa ufanisi.

*Wawezeshaji (Taifa, Wilaya na Kata).*

Matokeo mazuri ya mchakato wa upangaji mipango shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo yatatokana na kiwango cha uelewa cha wawezeshaji pamoja na stadi zao za uwezeshaji. Kutokana na uelewa wa wawezeshaji wa zoezi hili, Jamii itapata maarifa ya kutosha na kuweza kuandaa mipango bora. Nguvu zaidi inahitajika kuwaandaa wawezeshaji wa kitaifa, Wilaya na wale wa ngazi ya Kata kuhakikisha kuwa wanauelewa vizuri mchakato na hatimaye wanapata uwezo wa kuwezesha kwa ufanisi. Uewelewa wa wawezeshaji juu ya kuishirikisha Jamii katika kupanga ni mdogo, na zaidi umejikita katika minu za zamani na hasa ya PRA (Participatory Rural Apprisal). Kwa hiyo ni muhimu kuwapatia mafunzo ya kina juu ya mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo, pamoja na stadi za uwezeshaji.

## 3.5 Mapitio na Uwezeshaji

Zoezi la kueneza mfumo wa linafanyika mara moja katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Jamii inawezeshwa kuandaa mipango yao ya maendeleo. Hata hivyo kwa miaka ijayo mipango ya Jamii haina budi kufanyiwa Mapitio, ili kuendana na hali ya mahitaji ya Jamii na mabadiliko ya vipaumbele vyao. Haya yanafanyika wakati wa mapitio ya mipango ya Jamii. Mapitio ni mchakato wa kuhuisha mipango iliyopo kwa kushirikisha Jamii husika kulingana na taarifa zilizotokana na ufuatiliaji na tathmini na hali halisi ya utekelezaji wa mipango. Mchakato huu ni muhimu ufanyike kila mwaka. Wakati wa Mapitio mabadiliko ya sera yazingatiwe.

Uwezeshaji unahusu jitihada za Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuwezesha na kujengea Jamii uwezo wakati wa kutekeleza mipango yao ya maaendeleo. Uwezeshaji huu ni wa kitaalam, kifedha, usambazaji wa taarifa hasa zinazohusu sera za Taifa, mikakati mbalimbali, sera za kisekta na miongozo mbalimbali. Zaidi ya hayo, Jamii inawezeshwa kupanga upya, kutekeleza na kufanya ufuatiliaji na tathmini shirikishi. Katika kufanya haya ni muhimu Mamlaka za Serikali za Mitaa kusisitiza kuwa suala la umiliki wa mipango ni la Jamii yenyewe. Faida za Mapitio na uwezeshaji ni pamoja na Jamii kumiliki mchakato, kufahamu vipaumbele vya wakati uliopo, sera za kitaifa za kisekta na hatimaye kuiwezesha Jamii kutumia vizuri rasilimali zilizopo.

## 3.6 Dhana zinazotumika katika Mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo

<u>Maana ya Fursa</u>

*Fursa ni Rasilimali zilizopo katika Jamii ambazo ama zitatumika kikamilifu au hazitumiki. Fursa yawezwa kuanishwa kama:*

- Kile tulichonacho na tunakitumia vizuri kama huduma za afya (zahanati)
- Kile tulichonacho lakini hatukitumii vizuri kama ardhi inayofaa kwa kilimo cha kahawa lakini haitumiki
- Kile tulichonacho lakini hatukitumii kabisa kama hifadhi ya misitu yenye miti ya kuzalisha mbao ambao hautumiwi na Jamii
- Hatunacho lakini tunayo haki ya kukitumia. Kama Haki ya kutumia maji safi na salama lakini hayapatikani

Maana ya Vikwazo

Vikwazo ni vipingamizi vya matumizi ya fursa za maendeleo katika Jamii kwa mfano

- Vikwazo vya kijamii kama vile mila na desturi zilizopitwa na wakati
- Vikwazo vya kiuchumi kama vile ukosefu wa mitaji ya uwekezaji na uendeshaji
- Vikwazo vya kisiasa kama vile tofauti za itikadi
- Vikwazo vya kitaalam kama vile ukosefu wa wataalam wenye ujuzi.

*Baomantiki*

Baomantiki ni mtiririko wa mawazo yenye mantiki yanayotegemeana yaliyoandikwa katika jedwali kwa madhumuni ya kufikia malengo yaliyotarajiwa.
Baomantiki linaundwa na safu-wima zenye vipengele vifuatavyo;

- **Malengo mahususi:** Yanatokana na takwimu za upili na zile zilizokusanywa kutokana na zana shirikishi.
- **Fursa:** Ni rasilimali ambazo zikitumika vizuri zinawezesha kufikiwa kwa malengo mahususi.
- **Vikwazo:** Vinazuia fura zisitumike ipasavyo.
- **Sababisho:** kiini cha kuwepo kwa vikwazo.
- **Ufumbuzi:** Unaondoa vikwazo vilivyopo
- **Hatua za utekelezaji:** Shughuli zinazokabiliana na sababisho.
- **Mahitaji:** Rasilimali zinazohitajika kuwezesha hatua za utekelezaji kutekelezeka.

## 4.0 MCHAKATO WA KUANDAA MIPANGO SHIRIKISHI JAMII KWA MFUMO WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO

### 4.1 Itifaki ya Kuingia katika Jamii na Maandalizi ya Kijamii

Kabla ya kuanza zoezi la kuandaa Mpango Shirikishi Jamii, ni vema kuzingatia itifaki ya kuingia katika Jamii. Itifaki hizi ni pamoja na utoaji taarifa kwa viongozi katika ngazi mbali mbali (Wilaya, Kata, na Kijiji) kuhusu zoezi la uandaaji Mpango Shirikishi.

Mchoro wa kikombe cha Jamii unatumika kama kielelezo cha namna ya kuingia katika Jamii.




Viongozi na watu mashuhuri husikilizwa na Jamii. Unapotaka kupeleka taarifa kwa Jamii zinazohusu shughuli inayotakiwa kufanyika, ni vizuri kuwasiliana na kuwaelewesha viongozi na watu mashuhuri kwanza; ili wao wasaidie kuelewesha wananchi. Mawasiliano ya barua kwa viongozi wa Halmashauri ya Kijiji yafanyike kabla ya ziara ya maandalizi.

Utoaji taarifa unasaidia viongozi na wananchi kufahamu umuhimu wa zoezi hili na kushiriki kikamilifu. Aidha taarifa za awali zinasaidia kujenga mahusiano ya karibu kati ya wawezeshaji na Jamii.

Unapoingia katika Jamii tegemea kupata mwitikio tofauti wa makundi mbalimbali ya Jamii kama inavyoonyeshwa kwenye mchoro wa mwitikio wa Jamii.

**Mchoro wa mwitikio wa Jamii**




Kwa kawaida katika Jamii kuna makundi mbalimbali ya watu ambayo huwa na mwitikio tofauti wa masuala mbalimbali ya maendeleo kama ifuatavyo:

- Wanaokubali mabadiliko mapema; hawa ni wachache na huwa mfano kwa wengine
- Wafuasi, mara nyingi hawa ndio wako wengi katika Jamii; na
- Wanaochelewa kukubali mabadiliko - hawa wanapenda mabadiliko ya pole pole. Hawa wanaochelewa kukubali mabadiliko sio wapinga mabadiliko bali ni watu ambao bado hawajaelewa mabadiliko yenyewe yanayotakiwa.

**Maandalizi ya Jamii ngazi ya Kijiji/Kata**

**Lengo:** Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Jamii juu ya mpango shirikishi, Faida za kuwa na mpango shirikishi, na umuhimu wa kuunganisha nguvukazi katika maendeleo. Pia kusisitiza uwajibikaji wa viongozi wa Jamii na Jamii yenyewe kwa ujumla katika suala zima la mchakato wa mipango.

**Dhana:** Ni muhimu Jamii kuelewa kuwa suala zima la mchakato wa mipango ni jukumu lao, na wao ndio wamiliki wakuu wa mipango hiyo. Hivyo wasiwe na fikra kwamba mipango hiyo wanapelekewa na utekelezaji unaweza ukakoma mara tu zoezi la uenezaji linapoisha.

**Maudhui na umuhimu wa maandalizi ya Jamii.**

Katika mchakato wa uandaaji mipango shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo, maandalizi ya Jamii ni hatua muhimu katika kuitayarisha Jamii kushiriki kikamilifu katika hatua zote za kupanga mipango ya maendeleo yao. Msingi mkuu katika upangaji wa mipango shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ni ushirikishaji. Hivyo ni muhimu Jamii kutayarishwa ili pawepo na ushiriki wa kutosha na kila mmoja aweze kutoa shauku yake. Aidha ni muhimu pia Jamii kuelezwa waziwazi juu ya suala la umilikaji wa mipango yao. Suala hili likieleweka vizuri kwao, watapanga na kutekeleza mipango yao kwa ufanisi.

**Umuhimu wa maandalizi ya Jamii**

Maandalizi ya Jamii yana umuhimu ufuatao:

1. Kuiwezesha Jamii kutambua mahitaji yao, vikwazo vilivyopo na uwezo walio nao kukabiliana navyo.
2. Kuhamasisha Jamii kushiriki kikamilifu kwa lengo la kutoa shauku zao.
3. Kujenga umoja katika Jamii.
4. Kuamsha ari kwa Jamii kutambua majukumu na wajibu wao katika maendeleo yao
5. Kujenga hali ya kujiamini katika Jamii na kwamba wanaweza kufikia maamuzi yao.
6. Kuwezesha Jamii kutambua mwelekeo wake.
7. Kuindaa Jamii katika kupokea na kukubali mabadiliko yanayoweza kuwaletea maendeleo
8. Kuleta uaminifu miongoni mwa Jamii (kati ya Jamii na viongozi wao, kati ya Jamii na wawezeshaji na kati ya wawezeshaji na viongozi wa Jamii).

Kutokana na maelezo hayo, maandalizi ya Jamii yana nguzo muhimu zifuatazo;

- kujitambua kwa Jamii
- Juhudi za pamoja
- Kukubali mabadiliko kwa lengo la kupata matokeo chanya

Kwa hiyo maandalizi ya Jamii yanaweza kuangaliwa kwa mtazamo wa aina mbili. *Kwanza*, yanaweza yakachukuliwa kama ni hatua ya lazima kuindaa Jamii katika muda maalum, kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao. Katika hatua hii maandalizi ya Jamii yanahusisha mikutano ya maandalizi, uhamasishaji wa awali na usambazaji wa taarifa. *Pili*, kuwezesha Jamii kuwa tayari kujitambua na kuwa na juhudi za pamoja katika kukubali mabadiliko katika maendeleo. Mitazamo yote miwili inahusiana.

**Uhamasihaji na maandalizi kabla ya mchakato wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo**

Mchakato wa upangaji mipango shirkishi jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, utaanza kwa kufanyika kwa warsha ya uelewa kwa viongozi na watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, watu mashuhuri na viongozi wa siasa kwa muda wa siku mbili. Warsha hiyo itahusu Historia ya upangaji mipango, Maudhui ya mipango shirikishi, Mapitio na Uwezeshaji.[4] Mambo mengine yatakayowezeshwa katika warsha hiyo ni pamoja na Dira yaTaifa ya Maendeleo 2025 na masuala mtambuka. Ili kujenga uwezo wa uelewa kwa wa washiriki, warsha itaendeshwa kwa kuwasilisha mada, kazi kwa vikundi na majadiliano ya pamoja.

Katika ngazi ya Jamii mchakato wa maandalizi ya Jamii, utaanza kwa ziara ya maandalizi iliyotayarishwa vizuri. Kwa mchakato wa kijiini, ziara hii itafanyika kwa kukutana na Halmashauri ya Kijiji na kwa mjini mkutano wa maendeleo ya Kata. Katika mikutano hiyo wawezeshaji watafafanua mambo yote muhimu yanayohusu mchakato na kuandaa mazingira mazuri ya Jamii kushiriki.

Wawezeshaji, pia watawezesha washiriki kuelewa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ndiyo mwongozo wa jumla wa sera katika kuandaa mpango shirikishi, na kuweka vipaumbele kulingana na mahitaji na hali halisi ya Jamii husika.

Jambo lingine la muhimu, wakati wa ziara ya maandalizi ni majadiliano kati ya wawezeshaji na wajumbe wa H/Kijiji/Kata juu ya njia zitakazotumika kuhamasisha Jamii kabla ya Uzinduzi wa mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Njia tofauti zinaweza kutumika kutegemeana na Jamii yenyewe. Katika baadhi ya Jamii uhamasishaji unaweza ukafanywa kwa kutumia vikundi vya uhamasishaji Jamii vilivyopo kama vile, vikundi vya vijana na vikundi vya ngoma. Katika Jamii nyingine njia zinazotumika ni kama viongozi kutembelea kila kaya kutoa taarifa ya mkutano, mikutano ya vitongoji na kutoa matangazo kwa kutumia vipaza sauti.

Siku mbili zitatumika kuhamasisha Jamii kabla ya mkutano mkuu maalum wa uzinduzi wa mchakato. Mwezeshaji atafanya yote yaliyo ya muhimu katika hatua hii. Katika Jamii nyingine, vikundi vya sanaa kama vile vikundi vya ngoma vinaweza kutumika kama njia nzuri ya uhamasishaji. Kwa hali hii, katika siku ya kwanza ya uhamsishaji, wawezeshaji

[4] Mapitio na uwezeshaji vinajumuishwa katika warsha hii kwa sababu wakuu wa idara ambao ni miongoni mwa washiriki wa warsha wana jukumu kubwa katika mchakato wa mapitio na uwezeshaji.

watawezesha vikundi hivyo katika kufikisha ujumbe muhimu kwa Jamii katika siku inayofuata (siku ya pili). Masuala mengine ya kuwezesha katika vikundi hivyo ni kama;

- Umuhimu wa mpango shirikishi Jamii
- Kualika Jamii kushiriki kikamilifu katika mkutano mkuu maalum wa uzinduzi wa mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.

Ni vema kuwezesha vikundi hivyo kwa umakini zaidi ili ujumbe ueleweke kwa urahisi na kufikishwa vizuri katika Jamii. Endapo kuna uwezekano, uwezeshaji na uhamasishaji unaweza kuanza siku ileile(ya kwanza) na kisha siku ya pili, kuendelea kusambaza taarifa kwa Jamii kwa kutumia mbinu mbalimbali zilizotajwa hapo awali.
Vikundi ya uhamashaji vitafikisha ujumbe kwa Jamii kwa kushirikiana na viongozi wa Jamii wakiwa ni waratibu pamoja na wawezeshaji.

### 4.2 Uzinduzi wa mchakato wa upangaji mpango shirikishi Jamii

Siku ya Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji wa uzinduzi wa mchakato ni siku maalum ya wawezeshaji kukutana na wanaKijiji wote. Lengo la mkutano wa Kijiji ni kuielezea Jamii madhumuni ya zoezi la kuandaa Mpango shirikishi Jamii kwa kutumia Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo na jinsi wananchi watakavyo shiriki na kukubaliana ratiba ya zoezi hilo. Aidha Jamii ipewe nafasi kuuliza maswali ili ufafanuzi wa kina utolewe na wawezeshaji.

Baada ya hayo,mkutano mkuu maalum wa Kijiji utafanya yafuatayo :

- kuunda makundi mahususi kwa kuzingatia uwakilishi wa vitongoji, rika na jinsi. Uundaji huu wa makundi usisahau uwakilishi wa makundi yaliyo katika mazingira magumu zaidi.
- Kuchagua wawezeshaji wa Jamii 6 -10, ambao wanajua. kusoma na kuandika, wanaokubalika na kuheshimika katika Jamii na wanaojituma katika shughuli za maendeleo.
- Kuchagua wachora ramani
- Kuweka vigezo vya kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya.
- Kuchora ramani ya Kijiji.
- Kukubaliana njia ya kupita wakati wa kataa ya njia(mchakato wa Kijijini tu).
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu katika kaya.

### 4.3 Ukusanyaji wa Takwimu

Ukusanyaji wa takwimu katika mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo, unaanza mara tu baada ya Jamii kupokea taarifa kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kawaida, barua ya taarifa juu ya mchakato inakuwa imeambatanishwa na fomu ya kukusanyia takwimu.[5] Fomu ya kukusanyia takwimu itakuwa kama mwongozo kwa viongozi wa Jamii kukusanya takwimu mbalimbali kabla ya mchakato kuanza. Ufafanuzi wa yaliyomo katika fomu hizi utatolewa na wawezeshaji wakati wa ziara ya maandalizi. Takwimu zitakusanywa kwa madhumuni ya kuandaa mpango shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Takwimu zitakusanywa na kuoneshwa kwa kutumia namba, chati, michoro n.k.

**Aina za Takwimu***:*

Kuna aina mbili za takwimu :-

1. *Takwimu za upili*

Takwimu ambazo zipo tayari kwenye kumbukumbu mbalimbali za Kijiji/Kata zinazopatikana kwenye rejesta ya Kijiji, mafaili, rejista za shule na taasisi.

2. *Takwimu za awali:*

Takwimu ambazo zinakusaywa kwa kutumia zana Shirikishi Jamii. takwimu za aina hii zimegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo hapa chini:

- Takwimu za mazingira
- Takwimu za Nyakati
- Takwimu za kijamii na kiuchumi

[5] **Fomu yakukusanyia takwimu ngazi ya Jamii inaoneshwa mwishoni mwa kitabu.**

### 4.3.1 Takwimu za Mazingira

Takwimu hizi zinaonyesha fursa zilizopo na vikwazo katika Jamii. Hizi ni pamoja na matumizi ya ardhi, mazao, sura ya nchi, mito, tasisi, udongo na misitu. Zana za kukusanyia takwimu hizi ni ramani ya Kijiji na kataa ya njia.

#### *4.3.1.1 Ramani ya Kijiji/Kata*

Ramani ya Kijiji/Kata huchorwa na kikundi cha ramani kinachochaguliwa katika mkutano mkuu kwa kutumia rasilimali zilizopo kama vile vijiti, mkaa, mawe, majani, majivu n.k. Ramani huchorwa ardhini na kisha kuhamishiwa kwenye karatasi au daftari. Ramani ya Kijiji/Kata huonyesha mambo muhimu ikiwa ni pamoja na Dira, mipaka, makazi, taasisi zilizopo, rasilimali mbalimbali na ufunguo wa ramani.




Kundi la wachoraji ramani ya Kijiji

**Ramani ya Kijiji cha Nrao Kisangara – Wilaya ya Hai**




## *4.3.1.2 Kataa ya Njia (kwa mchakato wa Kijijini tu)*

Baada ya ramani ya Kijiji kuchorwa washiriki hukubaliana kwa pamoja na wazoefu Kijijini ni maeneo yapi ya kupita wakati wa kataa ya njia (matembezi mkato). Matembezi haya hufanywa kwa kutembea kutoka pembe moja ya Kijiji (mfano kaskazini) hadi nyingine (kusini) au magharibi kwenda mashariki. Timu ya wawezeshaji hutembea kwa kushirikiana na wanaKijiji. Matembezi haya husaidia wataalamu kukagua sehemu zinazohitaji huduma maalumu. Hii huonyesha matumizi ya ardhi, matatizo yanayowakabili na njia za kutatua matatizo hayo. Kataa ya njia pia husaidia timu ya wawezeshaji kuweza kugundua iwapo kuna taarifa fulani zitakazojitokeza na kuwa na mahitaji ya kipekee wakati wa kutafuta suluhisho, mfano ukarabati wa vyanzo vya maji, barabara n.k.

**Kataa ya njia Kijiji cha Nrao Kisangara – Wilaya ya Hai**



| | Bondela lima | Kisangara | Bondela Okyoro | Nrao Juu | Kyungukyena |
|---|---|---|---|---|---|
| **Udongo** | Udongo mweusi na mwekundu kidogo | Mwekundu | Mwekundu | Udongo mwekundu | Udongo wa usena |
| **Uoto** | Miti ya asili kutotesha migomba, kahawa, majani | Miti ya asili, kuotesha mibuni, migomba na majani ya mifugo | Miti ya asili na kuotesha migomba na mibuni | Miti ya matunda, miti ya asili ya kuotesha mibuni, migomba, majani ya mifugo | Miti ya sili, migomba na mibuni kidogo na majani |
| **Shughuli** | Kilimo cha mboga, mahindi, miwa, viazi, majimbi n.k. | Kilimo cha mibuni na migomba | Kilimo cha mibuni na migomba | Kilimo cha mibuni, migomba na mboga | Kilimo cha mibuni na migomba kidogo |
| **Makazi** | Hakuna | Yapo | Hakuna | Yapo mengi | Hakuna |
| **Huduma** | Hakuna | Kanisa, shule, bonde la maji, mfereji, duka, barabara | Hakuna | Shule, ofisi ya kijiji, umeme, bomba la maji, mfereji, mashine ya kusaga, chama cha ushirika, duka na barabara | Mfereji |
| **Fursa** | Miti ya mbao matunda, mfereji, mto na ardhi | Miti ya mbao matunda, ardhi, nguvu kazi | Miti ya mbao, matunda, ardhi kidogo | Ardhi kidogo yenye rutuba, miti ya mbao, nguvu kazi kubwa, majani ya mifugo | Miti ya mbao na majani ya mifugo |
| **Vikwazo** | Eneo dogo la ardhi, | Ongezeko la wakaazi/ ongezeko la watu | Mteremko mkali | Ongezeko la makaazi/ msongamano wa watu | Mmomonyoko wa ardhi na mteremko mkali |

## 4.3.2 Takwimu za Nyakati

Takwimu za nyakati zinapatikana kutokana na matukio ya kihistoria na kalenda ya msimu.

### *4.3.2.1 Matukio ya Kihistoria*

Ni zana shirikishi inayowezesha Jamii kuchambua mlolongo wa matukio muhimu ambayo yalitokea. Jamii huainisha matukio makubwa ya kihistoria yaliyoyotokea, sababisho zake, athari zilizotokea(zenye manufaa na ziizosababisha hasara) na hatua zilizochukuliwa kurekebisha hali hiyo(ufumbuzi). Aidha zana hii huwezesha Jamii kujifunza namna ya kukabiliana na maafa/ janga/ tukio na kuiga mikakati inayofaa.

**Mfano wa Matukio ya Kihistoria katika Kijiji cha Kona**

| Mwaka | Tukio | Sababisho | Madhara/ Manufaa | Ufumbuzi/ Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| 1939 | Njaa | Nzige waliharibu mazao | • Upungufu mkubwa wa chakula<br>• Mifugo walikufa. | • Mifugo iliuzwa, ili kunua chakula.<br>• Kutumia kilimo cha umwagiliaji na kupanda mazao yanayokomaa mapema kama vile viazi na mbogamboga. |
| 1940 | Barabara ya lami kufika Kijijini | Kusafirisha nafaka kutoka mashamba makubwa ya Kilimanjaro magharibi. | • Usafiri rahisi na wa uhakika.<br>• Kuongezeka kwa uzalishaji na kuanzishwa kwa masoko mapya | |

### *4.3.2.2 Kalenda ya Msimu*

Kalenda ya msimu ni zana shirikishi inayotumika kuwezesha kutambua shughuli mbalimbali zinazofanyika katika Jamii katika kipindi maalum. Kwa kawaida kalenda huanzia Januari na kuishia Desemba. Lakini kwa maeneo ya Vijijini kalenda huanzia wakati wa msimu wa mvua ambapo hutofautiana kati ya eneo na eneo. Mwanzo wa msimu hutofautiana toka sehemu hadi sehemu kufuatana na shughuli zinazofanyika na wahusika.

- Kalenda ya msimu huonyesha taarifa nyingi mbali mbali katika kipindi maalum. Hulinganisha shughuli za ndani ya Jamii za kila mwezi, nje ya Jamii na sekta zingine. Huwezesha Jamii kujua mzunguko wa shughuli inayotakiwa ifanyike katika maisha yao ya kila siku. Vile vile husaidia kutambua ni kipindi gani cha matatizo au faraja katika mwaka wenye matukio ya kawaida.
- Ni muhimu kuhakikisha kwamba kalenda ya msimu inatayarishwa kwa kipindi ambacho Jamii inafikiria kuwa ni mwaka wa kawaida.
- Mifano ya matukio yanayoonyeshwa katika kalenda ya msimu ni pamoja na tabia ya nchi (joto, baridi, upepo, mvua n.k), upatikanaji wa chakula, maji, kipato, msimu wa kupumzika n.k. majadiliano yataongozwa na maswali kama vile "ni lini mnapanda mahindi?" au "ni kipindi gani mnavuna?".

| **Kalenda ya msimu- Kijiji cha Nrao kisangara** | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Maelezo** | J | F | M | A | M | J | J | A | S | O | N | D |
| **1. Hali ya hewa** | | | | | | | | | | | | |
| Mvua | | | | | | | | | | | | |
| **2.Shughuli za kilimo** | | | | | | | | | | | | |
| Kilimo cha mahindi | | | | | | | | | | | | |
| Kulima | | | | | | | | | | | | |
| kupanda | | | | | | | | | | | | |
| kupalilia | | | | | | | | | | | | |
| Kuweka mblea | | | | | | | | | | | | |
| Kuvuna | | | | | | | | | | | | |
| **3. kilimo cha ndizi/kahawa** | | | | | | | | | | | | |
| kupalilia | | | | | | | | | | | | |
| Kukata matawi | | | | | | | | | | | | |
| Kupuliza dawa | | | | | | | | | | | | |
| Kuvuna | | | | | | | | | | | | |
| **4. magonjwa ya binadamu** | | | | | | | | | | | | |
| Malaria | | | | | | | | | | | | |
| Vichomi | | | | | | | | | | | | |
| kuharisha | | | | | | | | | | | | |
| **5. Kilimo cha matunda na mbogamboga** | | | | | | | | | | | | |
| Nyanya | | | | | | | | | | | | |
| Parachichi | | | | | | | | | | | | |
| Mchicha | | | | | | | | | | | | |
| Kabeji | | | | | | | | | | | | |
| **6. Shughuli za Utawala** | | | | | | | | | | | | |
| Nguvukazi | | | | | | | | | | | | |
| Upatikanaji wa chakula | | | | | | | | | | | | |

### 4.3.3 Takwimu za Kijamii na Kiuchumi

Takwimu za kijamii na kiuchumi zinakusanywa kwa kutumia uchambuzi wa Taasisi,uchambuzi wa vyanzo vya mapato na matumizi,tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya, ramani ya umilikaji rasilimali kijinsia, shughuli za kutwa kijinsia,uchambuzi wa shughuli za kijamii na kiuchumi katika mazingira na makundi mahususi.

#### *4.3.3.1 Uchambuzi wa Taasisi*

Taasisi ni asasi yenye uongozi na madhumuni maalum inayotoa huduma katika Jamii.
Uchambuzi wa taasisi unaisaidia Jamii kujua maeneo ya kushirikiana na taasisi zilizoko ndani na nje kwa msingi wa utawala bora( kama vile utawala, kuzuia na kupambana na rushwa na uwazi), huduma inayotolewa, haki za kijinsia, inasaidiaje kuimarisha uchumi na kuendeleza tamaduni za Jamii.

Uchambuzi wa taasisi unaiwezesha Jamii na wawezeshaji:

- Kuzitambua taasisi na kazi ambazo zinafanya.
- Taasisi ambazo zinashirikiana na Jamii katika nyanja mbalimbali za maendeleo.
- Ushirikiano kati ya taasisi katika kuihudumia Jamii.
- Kupunguza maingiliano ya kazi.
- Husaidia kutambua taasisi ambazo haziko ndani ya Jamii, lakini zina umuhimu.

**Kielelezo: Mahusiano baina ya Jamii na Taasisi zilizo ndani ya Jamii**




Chapati ililiyowekwa katikati inatoa tafsiri kuwa, taasisi hiyo ina mahusiano ya karibu na Jamii. Na iliyowekwa mbali ni kinyume chake. Jamii itatafsiri umuhimu wa taasisi kulingana na ukubwa wa chapati taasisi ilivyopewa yaani; taasisi iliyopewa chapati kubwa zaidi ndiyo yenye umuhimu mkubwa zaidi katika Jamii na ile iliyopewa chapati ndogo inaonesha kuwa na umuhimu mdogo katika Jamii.

Matokeo ya uchambuzi wa taasisi za ndani:

**Jedwali 7: Taasisi na umuhimu wake**

| Taasisi | Shughuli | Umuhimu | Nafasi ya kimahusiano | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Kijiji | utawala | 1 | 4 | – Mikutano ya Kijiji haiitishwi<br>– Hakuna uwazi katika mapato na matumizi. |
| Msikiti | Elimu na Ibada | 2 | 1 | – Kutoa ushauri<br>– Wamejenga shule ya awali tu |
| Shule | Elimu | 3 | 2 | – Matokeo mazuri ya mitihani |
| Kanisa | Huduma za kiroho | 4 | 3 | – Wanatoa mafundisho ya maadili mema |

**Kielelezo: Mahusiano ya taasisi na taasisi za ndani ya Jamii**




Chapati zilizoungana zinaonesha kuwa Taasisi zina mahusiano katika kutoa huduma.

**Kielelezo: Mahusiano baina ya Taasisi zilizo nje na Jamii**




Taasisi za nje zenye mishale iliyo karibu na kitovu zina mahusiano ya karibu na Jamii na zile ambazo mishale inakomea mbali ni kinyume chake. Ukubwa wa chapati unaonesha umuhimu wa taasisi katika Jamii.

#### *4.3.3.2 Uchambuzi wa Shughuli za Kiuchumi na Kijamii katika Mazingira*

Shughuli za kiuchumi ni kama ifuatavyo; kilimo, uvuvi, ufugaji, na biashara. Kwa upande wa pili shughuli za kijamii ni kama usafi wa makazi, matumizi ya madawa ya pembejeo, ujenzi na sherehe.

**Shughuli kulingana na umuhimu**




Chapati kubwa inaonyesha kuwa shughuli husika ina umuhimu mkubwa zaidi kwa Jamii. Katika kielelezo, shughuli za kilimo (kilimo cha mazao na ufugaji), ndizo zenye umuhimu mkubwa zaidi kwa Jamii.

**Uhusiano wa shughuli za kiuchumi na kijamii na mazingira mazingira**




Chapati iliyo karibu zaidi na kitovu inaonyesha kuwa shughuli husika ina athari kubwa zaidi katika mazingira. Uchambuzi wa Mahusiano baina ya mazingira na shughuli za kiuchumi na kijamii unaweza kufanyika kwa kutumia jedwali kama inavyooneshwa hapa chini.

**Mahusiano baina ya Shughuli za Kiuchumi na Kijamii na Mazingira**

| Shughuli za Kiuchumi/Jamii zenye Athari kwenye Mazingira | Namna inavyofanyika | Athari | Ufumbuzi |
|---|---|---|---|
| Biashara ndogondogo | | | |
| Kilimo | | | |
| Ufugaji | | | |
| Uvuvi | | | |

### *4.3.3.3 Ramani ya Rasilimali Kijinsia*

Ramani ya rasilimali kijinsia ni zana shirikishi inayotumika kuwezesha Jamii kubaini mapengo kijinsia juu ya umilikaji, utoaji maamuzi na nguvu kazi katika Kaya. Zana hii inawezesha Jamii kuibua masuala yanayohusu mapengo katika kumiliki rasilimali, mgawanyo wa kazi na majukumu kati ya wanaume, wanawake na watoto.

Ramani ya rasilimali kijinsia inasaidia kuainisha mapengo ya kijinsia ili kurekebisha hali hiyo. Ramani hii inasaidia kuamua ni nani ashiriki zaidi katika kazi fulani. Aidha ramani ya rasilimali kijinsia inasaidia kujifunza na kuelewa nani anamiliki na nani anatoa maamuzi, nani anatoa nguvu kazi, na nani anawajibika juu ya rasilimali katika Kaya.

**Kielelezo cha ramani ya rasilimnali Kijinsia**

| **Ng'ombe** | **Nyumba** | **Baiskeli** |
|---|---|---|
|  U<br>M<br>N |  U<br>M<br>N |  U<br>M<br>N |
| **Wanyama Wadogo** | **Shamba** | |
|  U<br>M<br>N | U<br>M<br>N  | |
| **Radio** | | |
| U<br>M<br>N  | | |

Ufunguo:
U = Umilikaji
M = Maamuzi
N = Nguvu kazi

**Jedwali la ramani ya rasilimali kijinsia**

| Rasilimali | Umilikaji | | Maamuzi | | Nguvukazi | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke |
| Ng,ombe | √ | | √ | | √ | √ |
| Nyumba | √ | | √ | | √ | √ |
| Baiskeli | √ | √ | √ | | √ | √ |
| Sungura/ Kuku | √ | | √ | | | √ |
| Radio | √ | | √ | | √ | √ |
| Mazao | √ | | √ | | √ | √ |
| ***Jumla:*** | ***6*** | ***1*** | ***6*** | ***0*** | ***5*** | ***6*** |

**Jedwali la majumuisho ya ramani ya rasilimali kijinsia**

| | Umilikaji | Maamuzi | Nguvu kazi |
|---|---|---|---|
| KE | 1 | 0 | 6 |
| ME | 6 | 6 | 5 |

Baada ya Jamii kubainisha mapengo ya kijinsia, hatua za kurekebisha ziainishwe na kuingizwa kwenye mpango.

### *4.3.3.4 Shughuli za Kutwa Kijinsia*

Shughuli za kutwa kijinsia ni zana shirikishi ambayo inasaidia kuibua mapengo ya kijinsia. Shughuli nyingi katika Jamii zinaongozwa bila kujali jinsia. Hapo awali kulikuwa na shughuli ambazo zilitengwa maalum kwa ajili ya jinsi ya kike kama vile kuchota maji, kutwanga, kupika, kuogesha watoto n.k. Hivi sasa watu wengi wameanza kuona umuhimu wa kuhusisha mipango na kazi ili kusaidiana bila kujali jinsi.

Hata hivyo katika Jamii zingine mgawanyo wa shughuli za jinsia bado unaendelea. Kwa maana hiyo, ni muhimu timu ya wawezeshaji kuwa makini ili isionekane inaingilia mila na desturi za Jamii hiyo. Kwa upande wa pili ni lazima kuwa makini na kazi maalumu za jinsia ili mipango mipya inayoanzishwa isizidi kugandamiza kundi ambalo tayari linafanya kazi nyingi.

Kuanzisha uhamasishaji katika ukusanyaji wa takwimu kunasaidia Jamii yenyewe kuanza kuangalia, ni wanaume au wanawake wanaofanya kazi nyingi za maendeleo katika mfumo wa mila na desturi zilizopitwa na wakati. Je kuna mabadiliko yeyote mazuri au kushutumu yaliyotokea katika shughuli za wajibu wa jinsia bila kuathiri Jamii. Ni nani aliyeanzisha mabadiliko hayo, Haya ni baadhi ya maswali ambayo wanaKijiji wanapaswa kujiuliza katika zoezi la kukusanya takwimu na hata wakati wa kupanga mipango yao ya baadaye.

**Namna ya kufanya Zoezi Hili**

WanaKijiji wanaume, wanawake, vijana kwa wazee wanagawanyika kijinsi. Timu ya wawezeshaji na wataalamu wa ugani watagawanyika kulingana na jinsi wakati wakiwa kwenye vikundi. Timu ya wawezeshaji watawezesha majadiliano na siyo kuchukua nafasi ya Jamii. Ni vema kuwakumbusha kuwa madhumuni mazima ya mazoezi haya ni kupata taarifa ambazo baadaye watazitumia katika kupanga mipango yao ya maendeleo kwa kutumia Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.

Majadiliano huria kuhusu suala la jinsia ni kitu nyeti katika Jamii nyingi. Baadhi ya Jamii kama hazikuelewa inawezekana kupokea mawazo haya kwa hisia potofu kwamba wataalamu wa nje wanawaingilia katika mambo yao au wanadharau mila zao. Ni vema kama wanaKijiji wenyewe watapewa nafasi ya kuongoza majadiliano ya jinsia baada ya kuelekezwa nini kinatakiwa kufanyika. Timu ya wawezeshaji inatakiwa kuwawezesha wanaKijiji Kuandaa ratiba ya kazi za siku kijinsia katika makundi.

Kila kikundi kitafanya majadiliano ya ratiba, kuanzia wakati wa kuamka asubuhi hadi wakati wa kwenda kulala usiku, Shughuli hizi ziandikwe kwenye manila kubwa. Baada ya vikundi kumaliza zoezi, wataweka pamoja ili kulinganisha kazi za jinsi ya kike na kiume kwa siku. Majadiliano ya wazi yaruhusiwe ili wanaKijiji watoe maoni yao na hatimaye kufikia muafaka. Timu ya wawezeshaji kwa njia hii itawezesha vikundi kufahamu nini wajibu wa Jamii katika suala la jinsia.

Kalenda ya kazi ya siku kwa jinsia inatoa picha ya nani anafanya nini katika Jamii. Aidha inasaidia kutoa picha wakati wa uandaaji wa mpango wa Kijiji. Timu ya wawezeshaji hutumia takwimu kuwakumbusha wanaKijiji wakati wa kuandaa Mpango Shirikishi Jamii, kwa kuwaeleza nini, na jinsi gani imefanya nini ili waweze kuhusisha kwenye mipango yao. Kama inawezekana yale yanayoonekana ni mzigo kwa jinsi moja yaweze kudhibitiwa bila kusababisha usumbufu na kazi nyingi kwa jinsi nyingine.

**Jedwali Na. 10: Shughuli za kutwa kijinsia - Kijiji cha Diola**

| Muda | Baba | Mama | Mtoto wa kiume | Mtoto wa kike |
|---|---|---|---|---|
| 11.00 | Amelala | Ameamka na kutayarisha mlo wa asubuhi | Amelala | Ameamka |
| 11.00 – 12.00 | Amelala | Amefuata maji | Amelala | Amefuata maji |
| 12.00 – 01.00 | Ameamka | • Anafanya kazi za usafi wa mazingira<br>• Kuchemsha maji ya kuoga<br>• Kuandaa kifungua kinywa | Ameamka | Anasafisha vyombo |
| 01.00 – 01.30 | Kifungua kinywa | Kifungua kinywa | Kifungua kinywa | Kifungua kinywa |
| 01.30 – 07.00 | Kufanya kazi za shambani | Kufanya kazi za shambani | Kwenda shule | Kwenda shule |
| 07.00 – 08.00 | Shambani | Anatafuta mboga/ kuni | Shule | Shule |
| 08.00 – 09.00 | Kurudi nyumbani | Kurudi nyumbani akiwa na mzigo wa kuni | Kurudi nyumbani | Kurudi nyumbani |
| 09.00 – 10.00 | Amepumzika | Anaandaa chakula | Amepumzika | Anamsaidia mama kuandaa chakula |
| 10.00 – 10.15 | Anakula | Anakula | Anakula | Anakula |
| 10.30 – 04.00 usiku | Burudani | • Kufua nguo<br>• Kuosha vyombo<br>• Kuangalia mifugo<br>• Kuogesha watoto<br>• Anatandika kitanda | Anacheza na kujisomea | Anaosha vyombo na kujisomea |
| 04.00 – 11.00 asubuhi | Amelala | Anaanda mlo wa asubuhi | Amelala | Amelala |
| Masaa ya kufanya kazi | 7:30 | 14 | 7:30 | 12 |

#### *4.3.3.5 Tathmini ya Uwezo wa Kaya*

Zoezi la kutathmini hali ya uwezo wa kiuchumi wa kila kaya kwenye Kijiji husika ni muhimu katika mpango shirikishi Jamii wa Kijiji. Zoezi hili huwezesha kutambua ni kaya ngapi au asilimia ngapi zina hali nzuri, nafuu, au dhalili (duni). Hili ni zoezi muhimu hivyo ni budi lifanywe kwa uangalifu. Watu wa nje na ndani ya Jamii wana mitazamo tofauti juu ya uwezo, maisha bora na kutokuwa sawa. Njia hii huzigawa kaya katika makundi kwa kufuata mitazamo tofauti ya uwezo/maisha bora. Lengo na madhumuni ni kufahamu kitu gani kinachomfanya mtu kuwa bora zaidi na mwingine kuwa duni. Njia hii inatoa fursa ya kufahamu mitizamo tofauti na maoni mbalimbali kuhusu uwezo au maisha bora kutoka wakazi wa kaya husika yenye hali tofauti za maisha.

**Jinsi ya kuendesha zoezi la tathmini ya uwezo**

Zoezi la tathmini ya uwezo litafanyika katika ngazi ya kitongoji. Washiriki wabainishe makundi matatu ya uwezo wa kujikimu katika Jamii yaani kundi la hali duni, nafuu na nzuri. Baada ya hapo washiriki watabainisha vigezo vya uwezo wa kujikimu kwa kila kundi. Baada ya kupata vigezo waombe wachague kutoka miongoni mwao wenzao wanne, wanawake wawili na wanaume wawili lakini wawe wale wanaowafahamu wakazi wote.

Kisha toa maelezo kwa ufasaha namna ya kutekeleza zoezi hilo.

Kila mkuu wa kaya atawekewa alama na wote hao wanne. Alama ni 1 – 5. Kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini

| | | |
|---|---|---|
| Kaya yenye hali Duni | Alama | 1 – 2 |
| Kaya yenye hali Nafuu | Alama | 3 |
| Kaya yenye hali Nzuri | Alama | 4 – 5 |

Chukua orodha ya wakuu wa kaya wa kitongoji, kisha waelekeze wale wawakilishi 4 kuwa wao ndio watakaoweka viwango kwa kila mmoja kwa kadri anavyofahamu na kufuata vigezo vilivyowekwa. Mfano ufuatao hapa chini unaonyesha baadhi ya vigezo vya uwezo wa kujikimu katika Kijiji cha Egeya

*Kaya yenye hali Nzuri*

- ⇨ Inayo nyumba iliyojengwa kwa tofali na kuezekwa kwa bati
- ⇨ Inayo baiskeli
- ⇨ Inayo radio
- ⇨ Inalo shamba la migazi 200 – 300
- ⇨ Inapata milo 3 kwa siku

*Kaya yenye hali Nafuu*

- ⇨ Inayo nyumba iliyojengwa kwa miti na kuezekwa kwa bati
- ⇨ Inayo radio ya mkulima
- ⇨ Inalo shamba la migazi 50 – 150
- ⇨ Inao weza kununua vitenge/ khanga
- ⇨ Inao uwezo wa kupata milo miwili kwa siku

*Kaya yenye hali Duni*

- ⇨ Haimiliki shamba
- ⇨ Inayo nyumba duni
- ⇨ Haina uhakika wa mlo wa siku
- ⇨ Haina uwezo wa kununua sare za shule

Andaa jedwali la tathmini ya Kaya kiuwezo

**Jedwali 1: Tathmini ya kaya kiuwezo – kitongoji cha Diola**

| **Na.** | Mkuu wa kaya | **Waweka alama** | | | | **Jumla** | **Hali** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **1** | **2** | **3** | **4** | | |
| 1 | Idd | 1 | 2 | 1 | 2 | 6 | Duni |
| 2 | Ramadhani | 5 | 4 | 5 | 4 | 18 | Nzuri |
| 3 | Doto | 3 | 2 | 4 | 2 | 12 | Nafuu |

Matokeo ya wastani ya uwezo wa kujikimu kwa kila kundi
Kaya zenye hali duni hupata alama kati ya 4 – 8
Kaya zenye hali nafuu hupata alama kati ya 9 – 15
Kaya zenye hali nzuri hupata alama kati ya 16 – 20

Kwa mgawanyo huu kaya zote zitafahamika ki– uwezo. Uzoefu umeonyesha kundi 2 na 3 hufanana sana kwa sababu kundi nafuu mara nyingi liko kwenye mpito kuelekea hali nzuri. Matokeo ya kila kitongoji hukusanywa na kujumlishwa na hivyo kuwezesha kupatikana matokeo yote ya Kijiji ambapo asilimia na idadi ya kaya kiuwezo hupatikana.

Andaa Jedwali la tathmini ya Kaya kiuwezo kama inavyooneshwa hapa:

**Jedwali 2: Tathmini ya jumla ya uwezo wa kukijimu wa kaya Kijiji cha Egeya**

| Na. | Kitongoji | Kaya | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Duni | Nafuu | Nzuri | Jumla ya kaya |
| 1 | Diola | 30 | 10 | 5 | 45 |
| 2 | Bwela | 52 | 27 | 13 | 92 |
| 3 | Uhundo | 67 | 22 | 10 | 99 |
| 4 | Magema | 43 | 17 | 9 | 69 |
| | **Jumla** | **192** | **76** | **37** | **305** |
| | **Asilimia** | **63** | **25** | **12** | **100** |

Uchambuzi wa tathmini ya uwezo wa kujikimu katika Kijiji cha Egeya umeonyesha kuwa asilimia 63 ya wanaKijiji wote wana hali duni, asilimia 25 wana hali nafuu, na asilimia 12 tu ndiyo wenye hali nzuri. Kwa kutumia mgawanyo huo wa kaya andaa makundi mahususi kwa ajili ya kutumika wakati wa kuendesha majadiliano mbalimbali ya ushirikishaji Jamii. Ni vizuri pia kupambanua zaidi kaya zilizo na hali duni zikafahamika, mbali ya idadi yake katika kitongoji. Pia kujua kaya zinaongozwa na watu mbalimbali kama: wafiwa wajane, mtoto yatima, vikongwe, wanaume na wanawake

**Jedwali Na. 3: Tathmini ya jumla ya uwezo wa kaya kwa kuzingatia kaya zenye hali duni**

| Kitongoji | Idadi ya kaya | Mkuu wa Kaya | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | Mjane | mfiwa | Kikongwe | | Watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi | |
| | | | | | | Me | Ke | Me | Ke |
| Bwela | 52 | 20 | 32 | 6 | 8 | 6 | - | 4 | - |
| Diola | 30 | 15 | 15 | 2 | 1 | 4 | - | 3 | - |
| Uhundo | 67 | 50 | 17 | 4 | - | 3 | - | 2 | - |
| Magema | 43 | 15 | 28 | 4 | 8 | 5 | - | 2 | - |
| **Jumla** | **192** | **100** | **92** | **16** | **17** | **18** | **-** | **11** | **-** |
| **Asilimia** | **100** | **52** | **48** | **8** | **9** | **9** | **-** | **6** | **-** |

Ni muhimu kuelewa sababu zinazoambatana na kaya zinazoongozwa na Wajane, watoto walio katika mazingira magumu zaidi na Vikongwe kuwa katika hali duni.

**Umuhimu wa Tathmini ya Uwezo wa kujikimu**

- Kuelewa hali ya kiuchumi na ya kijamii ya Kijiji/ Kata
- Kutambua walengwa hasa kama kuna mikakati ya makusudi ya kupambana na umaskini.

***Angalizo:***
*Katika mchakato wa mjini, tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya inafanywa kwa kufuata vigezo vilivyowekwa katika mikutano ya mitaa/kanda ya uzinduzi wa mchakato. Hatua za kufuata ni kama zile zinazotumika wakati wa mchakato wa Kijijini. Lakini jumla ya kaya zilizomo kwenye Kata itapatikana kwa kuunganisha idadi ya kaya za kila Mtaa. Vilevile watakaochaguliwa kufanya zoezi hili sharti wawe wanamfahamu kila mkazi anayeishi katika Mtaa husika.*

## 4.4 Kuandaa Rasimu ya Mpango Shirikishi Jamii

Makundi mahususi ni makundi yanayoundwa kwa makusudi maalum kwa kuzingatia jinsi, rika, makundi yaliyosahaulika na uwakilishi wa vitongoji/mitaa, ili kuwezesha kuibua masuala ambayo hayangeweza kujitokeza kwenye mkutano mkuu wa Kijiji. Hivyo kundi mahususi ni zana shirikishi na nyenzo. Hutumika kama zana pale ambapo yanakusanya takwimu na pia hutumika kama nyenzo pale yanapoandaa mpango shirikishi Jamii kwa kuzingatia malengo ya Dira yaTaifa ya Maendeleo 2025 ambayo ni mwongozo wa jumla wa kisera.

Kwa kutumia takwimu zilizokusanywa kutokana na zana shirikishi na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, makundi mahususi yataandaa Rasimu ya Mpango ambayo itaonesha waziwazi yafuatayo:

- Jamii inataka kufikia nini (malengo mhususi).
- Rasilimali/taasisi ambazo zikitumiwa vizuri zitasababisha kufikiwa kwa malengo mahususi (Fursa).

Mambo yanayosababisha fursa isitumike vizuri (vikwazo)

- Sababu za kuwepo kwa vikwazo (sababisho).
- Hatua za kuchukua kukabiliana na vikwazo (ufumbuzi).
- Shughuli za kuondoa sababisho (hatua za utekelezaji).
- Rasilimali zinazohitajika kufikia hatua za utekelezaji (mahitaji).
- Makadirio ya gharama- Jamii inaweza kufanya nini na haiwezi kufanya nini ili kufikia hatua za utekelezaji (gharama).
- Njia za kupima mafanikio (viashiria).

MFANO WA RASIMU YA MPANGO SHIRIKISHI JAMII ILIYOANDALIWA NA MAKUNDI MAHUSUSI:

Kijiji __________ Kata____________
Wilaya_________ Mkoa____________

Lengo kuu: Kujitosheleza kwa chakula na uhakika wa upatikanaji wake.

| Lengo Mahsusi | Fursa | Vikwazo | Sababisho | Ufumbuzi | Hatua za utekelezaji | Mahitaji | Gharama Ndani | Gharama Nje | Viashiria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuongeza uzalishaji wa mahindi kutoka gunia 10 kwa sasa hadi gunia 15 kwa ekari ifikapo mwaka 2010 | Upatikanaji /kuwepo kwa pembejeo za kilimo(mbegu,mbolea na dawa za kuulia wadudu | Uelewa Mdogo juu ya Matumizi ya Pembejeo za kilimo | Upungufu wa huduma za ugani | Uboreshaji wa matumizi ya pembejeo za kilimo | Kupatikana kwa usafiri | Pikipiki, Mafuta, Oili, | | 1,150,000 50,000 | Idadi ya magunia ya mahindi yanayozalishwa kwa ekari |
| | | | | | Kuunda vikundi vya shughuli za kilimo katika vitongoji | | | | |
| | | | | | Kutayarisha mashamba darasa | Mbegu Posho ya Mtaalamu | 50,000 | 75,000 | |
| | | | | | Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa mboji (mbolea) | - Mbolea -Maji -Majani | 0 | 0 | |

## 4.5 Kikao maalum cha Halmashauri ya Kijiji

Kikao maalum cha Halmashauri ya Kijiji, kitaitishwa ili kupokea na kujadili Rasimu ya Mpango iliyoandaliwa namakundi mahususi chini ya uratibu wa Afisa Mtendaji wa Kijiji. Kikao hiki kitaweka vipaumbele vitakavyowezesha kuandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu.

### 4.5.1 Kuweka vipaumbele kwa malengo mahususi

Wakati makundi mahususi yanatayarisha Rasimu ya Mpango, malengo mahususi mengi hubainishwa lakini kutokana na uchache wa rasilimali, si rahisi kutekeleza malengo yote mahususi. Kwa minajili hiyo baada ya makundi mahususi kuandaa Rasimu ya Mpango, kikao maalum cha Halmashauri ya Kijiji kinakaa kuweka vipaumbele na kuandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu.

Uwekaji vipaumbele ni mchakato unaoshindanisha malengo mahususi yote yaliyo katika mpango shirikishi Jamii (Baomantiki) kwa kuzingatia umuhimu wake. Kuna zana nyingi za kutumia katika kuweka vipaumbele, baadhi ya zana hizo ni pamoja na;

- Kuweka vipaumbele kwa kupiga kura
- Kuweka vipaumbele kwa utashi
- Kuweka vipaumbele kwa mlinganisho kijozi

**Uwekaji vipaumbele kwa Mlinganisho Kijozi**

Mlinganisho kijozi ni zana shirikishi inayotumika kuweka vipaumbele kwa malengo mahususi katika mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Mchakato huu hufanywa na Halmashauri ya Kijiji/ Kamati ya Maendeleo ya Kata

Orodha ya malengo mahususi inaandaliwa na kuwekwa kwenye jedwali bila ya kuziba vyumba vinavyolingana kwanza. Bango la jedwali la mlinganisho kijozi linabandikwa mahala ambapo kila mshiriki katika kikao ataona. Malengo mahususi yatajwe tena kwa washiriki; ndipo zoezi la kuziba vyumba kwa kulinganisha lifanywe.

Mchakato wa kulinganisha au kupambanisha malengo mahususi mbalimbali hufanywa kwa kulinganisha kila lengo mahsusi na malengo mengine yote. Zoezi hili hurudiwa kwa kila lengo. Lengo mahsusi lilichaguliwa na kukubaliwa kwa kura nyingi huandikwa kwenye chumba husika cha jedwali. Mfano ufuatao unaonesha jisni ya kuweka vipaumbele kwa njia ya mlinganisho kijozi.

**Mfano wa jedwali la uwekaji vipaumbele kwa mlinganisho Kijozi**

| **Lengo mahsusi** | Kuongeza uzalishaji wa mahindi | Kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza kwa asilimia mia moja | Upatikanaji wa maji safi na salama | Kuongeza pato la kaya | *Alama* | *Nafasi* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuongeza uzalishaji wa mahindi | | Kuongeza uzalishaji wa mahindi | Kuongeza uzalishaji wa mahindi | Kuongeza uzalishaji wa mahindi | 3 | 1 |
| Kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza kwa asilimia mia moja | | | Kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza kwa asilimia mia moja | Kuongeza pato la kaya | 1 | 3 |
| Upatikanaji wa maji safi na salama | | | | Kuongeza pato la kaya | 0 | 4 |
| Kuongeza pato la kaya | | | | | 2 | 2 |

Mwisho kila lengo mahususi huhesabiwa na kuwekwa alama. Kisha kila mmoja hupewa nafasi kuanzia ya kwanza hadi mwisho. Kwa mfano huu kipaumbele cha kwanza kwa mlinganisho kijozi ni Kuongeza uzalishaji wa zao la Mahindi ndio lengo mahususi la kufikia shabaha ya kujitosheleza kwa chakula.

Mlinganisho kijozi ni zana bora zaidi ya kuweka vipaumbele kwa malengo mahususi kwa kutumia Jamii nzima. Faida moja kuu ya kutumia zana ya mlinganisho kijozi ni kuwa inatoa fursa ya kulinganisha lengo moja mahususi na lingine hadi malengo mahususi yote yakamilike. Zana hii hutumia muda mrefu na hasa panapokuwepo na malengo mahususi mengi. Huhitaji uwezo mzuri wa uwezeshaji. Uwekaji vipaumbele ni zoezi muhimu ambalo linapaswa kufanyika kwa makini na uangalifu mkubwa.

**Uainishaji wa Mapato na Matumizi**

Vyanzo vya mapato ni muhimu katika uandaaji mpango na bajeti shirikishi katika ngazi zote za utendaji. Zoezi la kutambua vyanzo mbalimbali vya mapato katika Kijiji huanzia katika zoezi la makundi mahususi. Kwa kufanya hivyo wigo wa uchangiaji mawazo wa watu wengi katika kutambua vyanzo mbalimbali vya mapato ndani ya Jamii hupanuka. Pia huongeza uwazi na kupunguza mianya ya rushwa na ubadhirifu. Vyanzo vya mapato katika ngazi ya Kijiji/ Kata ni fedha na nguvu kazi zinazopatikana ndani na nje ya Kijiji.

**Mfano wa Jedwali la Uainishaji wa vyanzo vya Mapato na Matumizi**

| **Vyanzo vya mapato** | | **Matumizi** | |
|---|---|---|---|
| Vyanzo vya Mapato: | | (i) Utawala: | |
| (i) Vyanzo vya ndani | | Gharama za mikutano | 100,000 |
| Kodi | 1,000,000 | WDC | 200,000 |
| Ushuru | 1,200,000 | Uchunguzi na usafiri | 500,000 |
| Ada ya vinywaji vya kienyeji | 800,000 | Shajala | 200,000 |
| Mchango wa chakula shuleni | 2,000,000 | Tukrima | 600,000 |
| Ada ya mchanga | 2,500,000 | Mwenge wa uhuru | 500,000 |
| **Jumla ndogo:** | **7,500,000** | **Jumla ndogo:** | **2,100,000** |
| (ii) Vyanzo vya nje | | (ii) Maendeleo | |
| Mchango wa Halmashauri | | Chakula cha wanafunzi Shule ya msingi | 2,000,000 |
| Madarasa 2 | 1,000,000 | Ujenzi wa darasa na nyumba ya walimu (Halmashauri 2,000,000 na Halmashauri ya Kijiji/ Kata | 1,000,000<br>500,000 |
| TASAF | 2,000,000 | | |
| **Jumla ndogo**: | **3,000,000** | Zahanati :<br>- TASAF<br>- Halmashauri Kijiji/ Kata | 2,000,000<br>600,000 |
| (iii) Mapato yasiyokuwa ya fedha | | Uzalishaji wa mahindi | 1,400,000 |
| Nguvu kazi | 1,100,000 | Jumla ndogo: | 9,500,000 |
| ***Jumla kuu:*** | ***11,600,000*** | ***Jumla kuu:*** | ***11,600,000*** |

Makadirio ya makusanyo ya mapato kutoka vyanzo mbalimbali huonyesha kiwango cha uwezo wa Kijiji/ Kata kuweza kugharimia baadhi ya miradi yake ya maendeleo.

### 4.5.2 Halmashauri ya Kijiji kuandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu

Kikao maalum cha Halmashauri ya Kijiji ndicho kitakachopokea taarifa za mpango zilizojadiliwa na kuandaliwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji kwa kushirikiana na makundi mahususi. Kikao hiki ndicho kitakachoandaa Rasimu ya Mpango shirikishi Jamii. Washiriki katika kikao cha Halmashauri ya Kijiji wataweka vipaumbele kwa mpango mzima. Mara baada ya kuweka vipaumbele, Halmashauri ya Kijiji itaaandaa mpango wa miaka mitatu.

Takwimu muhimu katika zoezi hili ni vyanzo vya mapato vya Kijiji ikiwa ni pamoja na fedha zinazokusanywa na Kijiji chenyewe, fedha zilizoahidiwa na washirika wa maendeleo na nguvu kazi.

Anza na Mipango iliyo katika kipaumbele cha kwanza. Jamii ichambue kupata mipango ya mwaka wa kwanza kwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Mipango ambayo inayekelezwa na Jamii bila gharama yeyote. Mingi ya mipango hii ni ile ambayo inaendelea mwaka hadi mwaka. Kwa mfano – kuchemsha maji ya kunywa au kuchangia chakula cha watoto wa shule, au usafi wa mazingira n.k.
2. Mipango ambayo utekelezaji wake uko ndani ya uwezo wa Halmashauri ya Kijiji kwa kuzingatia mapato ya Kijiji ama kwa kugharamia mpango mzima au kwa kushirikiana na washirika wengine kama Halmashauri ya Wilaya.
3. Mipango ambayo inahitaji utekelezaji wa haraka hata kama gharama zake zitatoka nje ya uwezo wa Kijiji, mipango ya namna hii mara nyingi ni michache.

Baada ya kupata mipango ya mwaka wa kwanza endelea kuchambua vipaumbele vinavyofuata ili kupata mipango ya mwaka wa pili na watatu.

Mipango inayobaki itafikiriwa wakati wa mapitio baada ya utekelezaji kila mwaka.
Mpango wa miaka mitatu, ndiyo utakaowasilishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Kamati ya Maendeleo ya Kata na mkutano mkuu wa Kijiji.

**Jedwali la Mpango wa miaka mitatu**

| **Lengo Kuu** | **Lengo** | **Lengo Mahsusi** | **kipaumbele** | **Hatua za utekelezaji** | **Mwaka 1** | | **Mwaka 2** | | **Mwaka 3** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Gharama ambazo Kijiji kinaweza kufanya | Gharama ambazo Kijiji hakiwezi kufanya | Gharama ambazo Kijiji kinaweza kufanya | Gharama ambazo Kijiji hakiwezi kufanya | Gharama ambazo Kijiji kinaweza kufanya | Gharama ambazo Kijiji hakiwezi kufanya |
| | | | | | | | | | | |

## 4.6 Kamati ya Maendeleo ya Kata

Itapokea na kujadili mipango wa miaka mitatu wa Vijiji vyake na kisha kutoa *ushauri* katika maeneo ambayo inaona yanafaa kuzingatiwa na kuainisha mipango inayotekelezwa na Vijiji kwa pamoja.

### 4.7 Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji

Utaitishwa mkutano mkuu maalum wa Kijiji wa kupokea, kujadili na kupitisha Mpango Shirikishi Jamii wa miaka mitatu. WanaKijiji watajadili na kupitisha mpango wao wakizingatia uwezo wao wa kirasilimali za ndani na za kutoka nje, muda, utaalam na majukumu mengine yaliyopo Kijijini. Mpango utakaopitishwa na mkutano huo ndiyo mpango wa Kijiji.

## 4.8 Muhtasari wa shughuli za utekelezaji kisekta ngazi ya Kata

Baada ya mpango wa Jamii kuidhinishwa, hatua inayofuata, ni kuandaa muhtasari wa shughuli za utekelezaji kisekta katika ngazi ya Kata. Muhtasari huu unatokana na hatua za utekelezaji zilizomo katika mipango ya Vijiji ndani ya Kata husika. Kazi hii itafanywa na Afisa Mtendaji wa Kata na maafisa wengine ngazi ya Kata. Ikiwezekana maafisa watendaji wa mitaa(kwa mchakato wa mjini) wanaweza kushiriki. Muhtsari wa shughuli za utekelezaji kisekta utajazwa katika fomu rahisi kama inavyooneshwa katika mfano ufuatao

**Mfano wa fomu rahisi ya muhutasari wa shughuli za utekelezeji kisekta ( inaandaliwa katika ngazi ya Kata).**

Kata …………………….
Wilaya …………………..
Mkoa ……………………
Sekta: Kilimo (5005)…………………

| Jina la Kijiji | Hatua zautekelezaji | | | | Mahitaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kuanzisha mashamba darasa | Kujenga mtandao wa umwagiliaji | Kuajiri wataalamu wa kilimo | Shughuli nyingine | | | | | |
| AA | | | | | | | | | |
| BB | | | | | | | | | |
| CC | | | | | | | | | |
| DD | | | | | | | | | |
| **Jumla** | | | | | | | | | |

Angalizo: Kwa mchakato wa mjini, mipango ya Jamii inatayarishwa katika ngazi ya Kata. Hivyo, fomu ya muhutasari wa shughuli za utekelezaji kisekta, itajazwa kutokana na hatua za utekelezaji zilizomo katika mpango wa Kata. Hapa chini, ni kielelezo kinachoonesha mfano wa fomu rahisi ya muhutasari wa shughuli za utekelezaji kisekta

### 4.9 Ufuatiliaji na Tathmini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Msingi wa ufuatiliaji na tathmini shirikishi ni watu. Ushirikishwaji unaweza ama wa watu wote, au wa uwakilishi. Ngazi za upimaji na tathmini shirikishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama zifuatavyo:

- Kijiji:
  - Kamati za Kudumu za halmashauri za Kijiji hukutana kila mwezi
  - Halmashauri za Kijiji hukutana kila mwezi.
  - Mkutano mkuu wa Kijiji hukutana kila robo mwaka
- Kata:
  - Kamati ya Maendeleo ya Kata hukutana kila robo mwaka.
- Halmashauri:
  - Kamati ya usimamizi na uendeshaji hukutana mara moja kila mwezi
  - Kamati za kudumu hukutana kila mwezi/ robo mwaka.
  - Baraza la madiwani hukutana kila robo mwaka

**<u>Usimamizi wa Ufuatiliaji na Tathmini</u>**
Kila ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ina wajibu wa kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zake.

<u>Ngazi ya Kijiji</u>
Afisa Mtendaji wa Kijiji ana wajibu wa kuhakikisha kuwa mpango wa maendeleo wa Kijiji unatekelezwa. Atafanya kazi na kamati za kudumu za Halmashauri ya Kijiji na kutoa taarifa kwa Halmashauri ya Kijiji na mkutano mkuu wa Kijiji. Afisa Mtendaji wa Kijiji atawasilisha muhtasari wa mkutano mkuu kwenye halmashauri ya Wilaya na kutuma nakala kwa Afisa Mtendaji wa Kata.

<u>Ngazi ya Kata</u>
Afisa Mtendaji wa Kata anawajibu wa kuhakikisha kuwa mipango ya Vijiji vya Kata yake inatekelezwa. Atafanya kazi na wawezeshaji wa Kata katika kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri. Aidha, atafuatilia na kuona kwamba mikutano ya kisheria ya Kijiji inafanyika. Afisa Mtendaji wa Kata atawasilisha taarifa za Vijiji kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata.

<u>Ngazi ya mamlaka ya Serikali za Mitaa</u>
Mkurugenzi wa halamashauri ataunda timu ya wawezeshaji wa Wilaya 12 – 15; watakaoongozwa na Afisa Mipango na Afisa takwimu wa halmashauri. Wajibu wa timu ya wawezeshaji ni kuratibu na kujenga uwezo wa wawezeshaji wa Kata ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya Jamii na kuijengea uwezo.

## KIAMBATISHO 1: MCHAKATO WA MJINI

## MCHAKATO WA MJINI WA UANDAAJI MPANGO SHIRIKISHI JAMII WA FURSA NA VIKWAZO KWA MAENDELEO

### Utangulizi

Mji ni eneo dogo linalokaliwa na watu wengi na lenye ushindani mkubwa wa matumizi ya rasilimali. Shughuli za kiuchumi na kijamii hutegemeana, ingawa zipo shughuli nyingine zinazowafurahisha wengi na wakati huo huo zinawakera wengine. Kwa mfano shughuli ya kiwanda cha ngozi ni faraja kwa walioajiriwa ndani na nje ya kiwanda; lakini ni kero kwa wakazi wanaozunguka kiwanda kwa sababu ya utoaji wake wa harufu na umwagaji taka ovyo kutoka kiwandani.

Maeneo ya mjini yanapata huduma nyingi nzuri za kijamii na kiuchumi. Hata hivyo siyo wakazi wote wananufaika na huduma hizo. Kutokana na mwingiliano wa shughuli Miongoni mwa watu wa mjini, na wingi wa shughuli za watu binafsi katika Jamii za mijini, husababisha iwe vigumu kuwa na umiliki wa huduma za pamoja.

Vilevile kutokana na wingi na utofauti wa shughuli za watu wa mijini, inakuwa vigumu kuwahamasisha kwa shughuli za pamoja. Hali hii husababisha mzigo wa uendeshaji na utoaji wa huduma kuachwa mikononi mwa mamlaka za miji. Wakati mwingine watu wa mijini wamekuwa na mtazamo usio sahihi, kuwa ni wajibu wa mamlaka za miji kutoa huduma kwa kuwa zinakusanya kodi na mapato mengine kutoka kwa watumiaji wa huduma hizo. Mtazamo huu unasababisha iwe vigumu kwa watu kujikusanya na kuchukua hatua za pamoja katika masuala yanayoihusu Jamii yao.

Katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni, ipo tofauti kubwa miongoni mwa wakazi wa mijini, ikilinganishwa na wale wa Vijijini. Hakuna tofauti kubwa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni miongoni mwa wakazi wa Vijijini. Tofauti hizi kati ya watu wa mijini na wale wa Vijijini zinasababisha tofauti kubwa katika mitazamo juu ya masuala mbali mbali. Pia kutokana na tofauti hizi ni vigumu kuanzisha wazo na mbinu mpya kwa maendeleo katika maeneo ya mijini. Kwa mtazamo huu, wawezeshaji lazima wawe waangalifu katika kuwezesha uelewa wa pamoja wa Jamii za mijini katika kuleta maendeleo. Jambo la muhimu ni kukubali kuwa Jamii zinao uelewa, na uelewa huo lazima uelekezwe katika maendeleo yao.

**Muundo wa Utawala**

Muundo wa utawala wa mji unatofautiana na wa Vijijini. Kisheria, mji umegawanywa katika maeneo ya mitaa na Kata. Mitaa ina Mwenyekiti; na baadhi ya Mitaa ina Maafisa Watendaji. Hata hivyo, Mtaa si Serikali kamili kisheria. Katika ngazi ya Kata za mijini kuna Kamati ya Maendeleo ya Kata ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kushughulikia maendeleo ya eneo lake. Wakati wa mchakato mkutano mkuu unaweza kuunaganisha mitaa miwili au zaidi na kuitwa kanda na mwenyekiti mmojawapo kati ya wenyeviti wa mitaa hiyo atakuwa ndiye mwenyekiti wa mkutano huu. Kwa kuzingatia mazingira ya mjini kama ilivyoelezwa hapo juu, Mchakato wa mjini ni tofauti na ule wa Vijijini.

**MCHAKATO WA MJINI**

***<u>Ziara ya maandalizi</u>***

Taarifa za ziara hii zinatakiwa kutolewa mapema kwa uongozi wa Kata na washirika wake wa maendeleo na kukumbusha siku chache kabla ya ziara kufanyika. Ziara hii ni kwa ajili ya kukutana na Kamati ya Maendeleo ya Kata; Watu maarufu, wakuu wa madhehebu na taasisi na washirika wa maendeleo walioko katika Kata. kwa kufanya hivyo inatarajiwa kuwa mahudhurio yatakuwa mazuri na washiriki watakuwa wachangamfu na wadadisi kutoa nuru ya kuzinduliwa na kuendesha mchakato wa mpango shirikishi Jamii kwa kutumia Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.

***<u>Mkutano wa Uzinduzi wa mchakato wa mjini</u>***

Kisheria Kata haina mkutano mkuu ila mitaa ina mikutano mikuu. Ili kufanikisha uzinduzi wa mchakato katika Kata, ni vema mitaa ikagawanywa katika kanda. Mitaa inayounda kanda moja itateua mwenyekiti mmoja wa Mtaa kuwa mwenyekiti wa Mkutano wa uzinduzi huo. Aidha, wawezeshaji wa Kata hiyo wajigawe katika kanda kwa ajili ya kuwezesha uzinduzi wa mchakato. Ili kurahisisha ugawaji wa kanda, ni vema kanda hizo zikagawanywa katika ziara ya maandalizi. Katika mkutano wa uzinduzi, kila kanda itateua wawakilishi wa kuunda makundi mahususi yenye uwakilishi wa kutosha kwa kuzingatia jinsi, rika na watu walio kwenye hali ngumu. Wawakilishi wa kanda watakusanyika katika Kata kuendesha mchakato. Kwa namna hii wananchi wote katika Kata watakuwa wameshiriki katika uzinduzi.

***<u>Kupitisha mpango</u>***

Hii ndiyo hatua ya kukamilisha mchakato mzima wa kuandaa Mpango Shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Afisa Mtendaji wa Kata atatayarisha Rasimu ya Mpango wa Kata kwa kushirikiana na makundi mahususi. Baada ya kukamilisha Rasimu

ya Mpango, Afisa Mtendaji wa Kata kwa kushirikiana na wawezeshaji wa Kata watajigawa na kuwasilisha Rasimu ya Mpango huo katika mikutano mikuu ya mitaa kikanda. Maoni yaliyotolewa na mikutano mikuu ya mitaa kikanda, yatajumuisha kwenye rasimu. Mwisho Rasimu ya Mpango itawasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa kuidhinishwa.

Afisa Mtendaji wa Kata atawasilisha Mpango ulioidhinishwa kwa Mkurugenzi wa Mji.

**Zana shirikishi zisizotumika katika mchakato wa mjini**

*Kataa ya njia*
Maeneo ya mjini yamepimwa na kujengwa; kwa hiyo fursa na vikwazo vimekwisha shughulikiwa katika Mpango wa mji. Aidha, katika maeneo ambayo hayajapimwa lakini yamejengwa sio rahisi kupitika.

*Matukio ya kihistoria*
Mjini kuna mpango mji. Kwa hiyo wakazi wa mjini hawawezi kujifunza kutokana na matukio ya kihistoria kupanga matumizi ya ardhi ya baadae. Pia wakazi wengi wa mjini ni wale wanaoingia na kutoka na shughuli zao hutofautiana na ni za muda.

## KIAMBATISHO II: RATIBA YA MCHAKATO WA KIJIJINI

**Siku ya Kwanza**

- Maandalizi ya kijamii.
  - Kukutana na wajumbe wa H/Kijiji.
  - Kutoa maelezo juu historia ya upangaji mipango ya Jamii
  - Kutoa maelezo ya upangaji mipango ya Jamii kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo.
  - kujadili na kukubaliana mbinu za kufanikisha mahudhurio ya mkutano Mkuu.
  - Uwezeshaji kwa vikundi vya kuhamasisha Jamii.
- Kukusanya takwimu

**Siku ya pili**

- Maandalizi ya Jamii (mwendelezo wa shughuli ya siku ya kwanza).
- Kuendelea kukusanya takwimu.

**Siku ya tatu**

- Mkutano mkuu maalum wa Kijiji wa uzinduzi wa mchakato
- Kuunda makundi mahsusi.
  - Wazee wa kike na wa kiume
  - Vijana wa kike na wa kiume
- Kuchagua wachora ramani.
- Kuchagua wawezeshaji wa Jamii (wawili kutoka kila kitongoji)
- Kuchora ramani ya Kijiji
- Kufanya tahmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya.

**Siku ya nne**

- Kataa ya njia
- Matukio ya kihistoria
- Ramani ya umilikaji rasilimali kijinsia.
- Uchambuzi wa taasisi.
- Kalenda ya msimu.
- Uchambuzi wa vyanzo vya mapato na matumizi
- Shughuli za kutwa kijinsia.

**Siku ya tano**

- Makundi mahsusi kujadili Dira ya Taifa ya maendeleo 2025

Lengo kuu: Maisha Bora na mazuri

- Kujitosheleza kwa chakula na kuwa na uhakika wa upatikanaji wake
- Elimu kwa wote
- Usawa wa kijinsia
- Upatikanaji wa hudumd ya Afya ya msingi kwa wote

**Siku ya sita**

- Makundi mahsusi kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025
  - Upatikanaji wa Huduma bora za uzazi kwa wote wenye umri unaostahili.
  - Kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa robo tatu ya viwango vya sasa.
  - Upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wote
  - Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati.
  - Kuondoa kabisa umasikini uliokithiri.

**Siku ya Saba**

- Makundi kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025(Uongozi bora na Utawala wa kisheria)
  - Maadili mema na kuthamini utamaduni
  - Uadilifu na kuheshimu utawala wa kisheria
  - Kuokuwepo kwa rushwa na maovu mengine
  - Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake

**Siku ya nane**

- Makundi mahsusi yanakutana kuunganisha rasimu ya kwanza ya mpango

**Siku ya tisa**

- H/Kijiji kuweka vipaumbele vya malengo mahususi .
- Kuandaa Rasimu ya Mpango wa miaka mitatu.

**Siku ya kumi**

- Kikao maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kufanyika ili kutoa ushauri kwenye rasimu ya mipango ya miaka mitatu ya Vijiji.

**Siku ya kumi na moja**

- Mkutano mkuu maalum wa Kijiji kupokea, kujadili na kupitisha mpango wa Kijiji

**Siku ya kumi na mbili**

- Kuandaa muhtasari wa shughuli za utekelelzaji kisekta kwa kutumia jedwali rahisi katika ngazi ya Kata.

## KIAMBATISHO III: RATIBA YA MCHAKATO WA MJINI

**Siku ya 1**

- Maandalizi ya Jamii
  - Mkutano wa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata.
  - Kuelezea historia fupi ya upangaji mipango
  - Kuelezea mchakato wa upangaji mipango kwa kutumia mfumo wa fursa na vikwazo.
  - Maandalizi ya mikutano mikuu ya kanda/mitaa.
  - Uhamasishaji wa mwanzo wa Jamii.
- Ukusanyaji wa takwimu

**Siku ya 2**

- Maandalizi ya Jamii (yanaendelea toka siku ya 1).
- Ukusanyaji wa takwimu.

**Siku ya 3**

- Mikutano katika kanda/mitaa ya uzinduzi wa mchakato wa mfumo wa fursa na vikwazo.
- Uchaguzi wa wawezeshaji wa Jamii ( 2 kutoka kila Mtaa ).
- Uundaji wa makundi mahususi.
  - Wazee wa kike na wa kiume
  - Vijana wa kike na wa kiume
- Uchaguzi wa wachora ramani

**Siku ya 4**

- Kuchora ramani ya Kata.
- Tathmini ya uwezo wa kujikimu wa kaya.
- Uchambuzi wa taasisi
- Shughuli za kutwa kijinsia.
- Ramani ya umilikaji rasilimali kijinsia.
- Uchambuzi wa vyanzo vya mapato na matumizi.

**Siku ya 5**

- Makundi mahususi kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (maisha bora na mazuri).

Lengo kuu: Maisha Bora na mazuri

- Kujitosheleza kwa chakula na kuwa na uhakika wa upatikanaji wake.
- Elimu kwa wote
- Usawa wa kijinsia
- Upatikanaji wa hudumd ya Afya ya msingi kwa wote

**Siku ya 6**
Makundi mahsusi kuendelea kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

- Upatikanaji wa Huduma bora za uzazi kwa wote wenye umri unaostahili.
- Kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa robo tatu ya viwango vya sasa.
- Upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wote
- Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati.
- Kuondoa kabisa umasikini uliokithiri.

**Siku ya 7**
Makundi kujadili Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Uongozi bora na Utawala wa kisheria)

- Maadili mema na kuthamini utamaduni
- Uadilifu na kuheshimu utawala wa kisheria
- Kutokuwepo kwa rushwa na maovu mengine
- Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake

**Siku ya 8**

- Makundi mahususi kuandaa Rasimu ya Mpango wa Kata.

**Siku ya 9**

- Mikutano ya mitaa/kanda ili kutoa maoni kuhusu Rasimu ya Mpango wa Kata.

**Siku ya 10**

- Afisa Mtendaji akishirikiana na makundi mahususi kujumuisha maoni nakuingiza kwenye mpango wa Kata.

**Siku ya 11**

- Kamati ya Maendeleo ya Kata kuweka vipaumbelekwa malego mahusi,kandaa na kupitisha mpango wa miaka 3.

**Siku ya 12**

- Kuandika shughuli zilizomo katika mpango na wa Kata katika jedwali rahisi kisekta.

## KIAMBATISHO IV: FOMU YA TAKWIMU

### 1.0 UTAWALA

1. Kata/Kijiji …………………………………………….
2. Eneo…………………….
3. Idadi ya Vitongoji/Mitaa/Vijiji ……………………………….
4. Wajumbe wa H/Kijiji: me…………… Ke …………..
5. Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata: me………ke……
6. Idadi ya wakazi:
    - Wanawake …………………………………
    - Wanaume ………………………………….
    - Wenye uwezo wa kafanya kazi me…………ke…………….
    - Watoto: me……………………….ke………………………
    - Yatima: me……………………….ke……………………….
    - Watoto wa mtaani me…………….ke……………………….
    - Walemavu: me…………………..ke………………………
    - Wajane ………………………………………………….
    - Vikongwe me …………………….ke……………………..

### 2.1 ELIMU YA MSINGI:

- Idadi ya watoto wote katika Kijiji/Kata wenye umri wa miaka 7 - 13
  Wasichana…………. wavulana ………………. Jumla……….
- Idadi ya wanafunzi walioacha shule (miaka 3 iliyopita)
  Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….
- watoto wa umri wa miaka 7 waliostahili kuandikishwa (miaka 3 iliyopita)
  Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….
- wanafunzi wa umri wa miaka 7 walioandikishwa (miaka 3 iliyopita)
  Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….
- Wastani wa mahudhurio ya wanafunzi shuleni kwa mwaka (miaka 3 iliyopita) Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….
- Kiwango cha umalizaji shule ya msingi (miaka 3 iliyopita)
  Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….
- Kiwango cha kufaulu (miaka 3 iliyopita)
  Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….

- Kiwango cha kujiunga na Elimu ya sekondari (miaka 3 iliyopita)
  Wasichana…………. wavulana………………. Jumla……….

- Idadi ya wanafunzi kwa chumba cha darasa………… upungufu wa madarasa uliopo……………….
- Idadi ya mikondo……………….
- Uwiano wa matundu ya choo me……../ke…….upungufu wa matundu ya vyoo ke……../me……..
- Idadi ya shule za msingi …………. Shule za Sekondari…………, Vyuo……….
- Nyumba za walimu zilizopo……………… na mahitaji……………
- Uwiano wa dawati kwa mwanafunzi………… upungufu wa madawati……….
- Upatikaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kama uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi…………………………….
- Shule za awali zilizopo……………………….

## 2.2. ELIMU YA WATU WAZIMA:

- Elimu inayotolewa( KCK, KCM, MEMKWA, MUKEJA n.k.)…………….
- Idadi ya waliojiandikisha kwenye Elimu ya watu Wazima
  Me……………. ke…………Jumla…………………
- Idadi ya wanaohudhuria darasa la Watu Wazima
  Me………………ke …………Jumla…………..
- Walimu wa kisomo cha watu wazima – idadi……………….
- Madarasa ya Elimu ya watu wazima - Idadi ………….
- Madarasa ya MEMKWA yaliyoanzishwa…………………………………………………… na idadi ya wanafunzi ………me…../ke…… waliojiandikisha.

## 2.0 AFYA:

- Magonjwa makuu yanayosumbua taja magonjwa na idadi
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
- Magonjwa ya mlipuko taja kama yalitokea na idadi(mwaka 1 uliopita)
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..

- Magonjwa ya kuambukiza taja magonjwa na idadi kwa <5 na >5

  **Chini ya miaka 5**

  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..

  **Zaidi ya miaka 5**

  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..
  Ugonjwa…………. idadi ya waliougua…………..

  - Huduma za afya zinazopatikana na umbali uliopo kutoka kwa Jamii:
    - Zahanati…………………umbali…………
    - Kituo cha afya…………..umbali………….
    - Hospitali ………………..umbali………….
    - Zahanati za Binafsi……… umbali………
  - Uhai wa kamati ya Afya
  - Idadi ya vyoo bora………..
  - Idadi ya wahudumu wa afya ya msingi katika Kijiji……….
  - Siku ya afya inavyoendeshwa Kijijini
  - Huduma ya kutembelewa Kaya

**3.1. HUDUMA BORA ZA UZAZI:**

- Idadi ya watoto chini ya mwaka 1
- Idadi ya watoto chini ya miaka 5……………….
- Hali ya lishe ya watoto chini ya miaka 5
  - Utapiamlo mkali (idadi)…………
  - Utapiamlo wa kati (idadi…………..

- Chanjo kwa watoto chini ya mwaka mmoja (waliostahili kuchanjwa na waliopata chanjo.)
  - BCG( idadi)………..
  - Polio 3 (idadi)………..
  - Donda koo na Pepopunda (DPT - HB3) (idadi)………..
  - Surua (idadi)………..
  - Vitamin A (idadi)………..
- Idadi ya watoto waliozaliwa na uzito pungufu (mwaka 1 uliopita)……………………..
- Idadi ya watoto waliozaliwa kabla ya wakati (mwaka 1 uliopita)……………..
- Watoto wanaozaliwa wafu (mwaka 1 uliopita) (idadi)………..
- Idadi ya vifo vya akina Mama vinavyotokana na uzazi (mwaka 1 uliopita) …………..
- Idadi ya wanawake wanaostahili kuzaa (19-45)……………..
- Idadi ya wanawake wanaozaa chini ya umri wa miaka (20) na zaidi ya miaka 35 (mwaka 1 uliopita)……………..
- Idadi ya waliopata chanjo (TT1) na kuendelea (mwaka1uliopita)……………..
- Huduma za uzazi zilizopo
- Idadi ya wanaotumia uzazi wa mpango
- Idadi ya wahudumu wa Afya ya Uzazi:
  - Wakati wa ujauzito
  - Wakati wa kujifungua
  - Baada ya kujifungua

**3.2. UKIMWI:**

- Vifo vilivyosababishwa na UKIMWI ( mwaka 1au 3 iliyopita)idadi………..
- Idadi ya waathirika – HIV (waliopimwa)……………..
- Kiwango cha maambukizo ya UKIMWI ……………….

**3.0 UPATIKANAJI WA MAJI SAFI NA SALAMA:**

- Vyanzo vya maji - orodhesha idadi ya visima, bomba, vyanzo vya
- maji vya asili
- Maji ya kutega: Idadi ya watu wenye visima vya maji ya kutega
- Umbali hadi kwenye vyanzo vya maji
- Idadi ya kaya zinazopata maji safi na salama
- Kamati za maji
- Mfuko wa maji

**5.0. HALI YA KIUCHUMI:**

- Wastani wa kipato kwa mwaka kwa:
  - Mtu……………
  - Kaya………..
  - Mtaa/Kijiji………….
  - Kata………………….
- Shughuli kuu za kujiletea kipato (taja)
- Taasisi zilizopo kwenye Kata/Kijiji (mwaka 1 uliopita))

**5.1. HUDUMA ZA KIUCHUMI:**

- Barabara; taja urefu km…………
- Vyanzo vya nishati(taja)
- Mawasiliano
  - wanaotoa huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi
  - huduma za posta.
  - Simu za mezani
  - Tovuti
  - Radio
  - Nukushi
  - Mtandao
  - Televisheni
- Soko la bidhaa na mazao
- Eneo la soko
- Huduma ya usafiri wa umma.

**6.0. SEKTA BINAFSI**

- Karakana za Ufundi/Gereji
- Viwanda vidogo
- Hotel/Migahawa
- Maduka
- Maduka ya madawa
- Vituo vya mafuta
- Vikindi vya uzalishaji
- Mashirika yasiyokuwa yaSerikali (NGOs)

## 7.0. KILIMO NA MIFUGO:

- Eneo linalofaa kilimo (ekari) ……………….
- Eneo linalolimwa (ekari) ……………. (kwa kila zao)
- Mazao makuu ya chakula (taja)
- Wastani wa mavuno kwa Ha ………… (magunia)
- Mazao makuu ya biashara (taja)
- Upatikanaji wa pembejeo za kilimo na mifugo
- Idadi ya vyama vya ushirika vya wakulima
- Idadi ya iwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo
- Hifadhi ya mazao (maghala, vihenge n.k)
- Idadi ya wafugaji
- Idadi ya mifugo
- Aina ya mifugo
- Eneo linalofaa kwa ufugaji (ekari) …………
- Magonjwa ya mifugo
- Idadi ya majasho
- Minada
- Idadi ya wataalamu wa kilimo na mifugo

## 8.0. MAZINGIRA:

Eneo la misitu Ekari ……………………
Idadi ya miti iliyopandwa………………
Idadi ya bustani za miche ya miti…………….